JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA


# MKAKATI WA UELIMISHAJI NA UHAMASISHAJI WA SENSA YA WATU NA MAKAZI YA MWAKA 2022



TANZANIA
SENSA
2022
Jiandae Kuhesabiwa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# MKAKATI WA UELIMISHAJI NA UHAMASISHAJI WA SENSA YA WATU NA MAKAZI YA MWAKA 2022




Ofisi ya Taifa ya Takwimu,
Wizara ya Fedha na Mipango,
S.L.P. 2683, 18 Barabara ya Jakaya Kikwete,
DODOMA, TANZANIA

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali,
Ofisi ya Rais- Fedha na Mipango,
S.L.P. 2321, Mtaa wa Mazizini,
ZANZIBAR

# SHUKRANI



Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 ni hitajio la moja kwa moja kutoka Kamisheni ya Takwimu ya Umoja wa Mataifa (United Nations Statistical Commission) linaloitaka kila Nchi kuandaa mwongozo wa kutoa elimu kwa watu wote kushiriki katika kutoa taarifa sahihi za kitakwimu za kidemografia, kijamii, kiuchumi na mazingira wanayoishi.

Lengo kuu la Mkakati huu ni kuelimisha na kuhamasisha watu wote kushiriki kikamilifu katika zoezi la Sensa na kuhakikisha kila mtu aliyelala ndani ya mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania usiku wa kuamkia Siku ya Sensa anahesabiwa na anahesabiwa mara moja tu. Taarifa zitakazopatikana zitaiwezesha Serikali na wadau kutunga Sera, kufuatilia na kutathmini malengo mbalimbali ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kama vile Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 -2025/26), Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano Zanzibar (2021/22-2025/26), Ajenda ya Maendeleo ya Afrika ya Mwaka 2063 na Ajenda ya Dunia ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030.

Mkakati huu umefafanua kwa kina nafasi, wajibu na majukumu ya kila mdau atakayeshirikiana na Serikali katika kutekeleza majukumu yaliyoainishwa katika ratiba nzima ya Sensa. Halikadhalika, Mkakati umelenga kuongeza uelewa kuhusu Sensa ya Watu na Makazi, utatumika pia kuhamasisha wadau wa ndani na wa nje ya nchi kuunga mkono juhudi za Serikali kwa kuchangia rasilimali fedha, vifaa na utaalamu ili kufanikisha utekelezaji wa Sensa.

Kwa msingi huo, sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote ambao walihusika na maandalizi ya mkakati huu. Hivyo basi, napenda kuishukuru Menejimenti ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa upande wa Tanzania Bara, Menejimenti ya Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, Wakurugenzi na Mameneja wote kwa pande zote mbili za Muungano.

Mkakati huu umeshirikisha wataalamu kutoka katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, hivyo, naishukuru Ofisi ya Mkurugenzi wa Idara ya Habari-MAELEZO na Msemaji Mkuu wa Serikali; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; Tume ya Taifa ya Uchaguzi; Ofisi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Zanzibar na wataalamu wengine binafsi.

Aidha, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru washiriki wote wa mkutano wa wadau wa habari waliojadili rasimu ya Mkakati huu kwa michango yao mbalimbali ikiwemo maoni na mapendekezo ambayo yameboresha kwa kiwango kikubwa ubora wa Mkakati huu.

Ni matarajio yangu kuwa, Mkakati huu utatumika kuongeza uelewa na hamasa kwa wadau wote wa Sensa na Wananchi kwa ujumla hivyo kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 na kufikia malengo yaliyopangwa katika utekelezaji wa zoezi hili la kitaifa.



**Samia Suluhu Hassan**

**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**Dodoma**

**Septemba, 2021**

# DIBAJI

Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 umeandaliwa mahsusi kama mwongozo wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar ili kutekeleza shughuli za Sensa kwa kuwashirikisha kwa kiasi kikubwa wadau na wananchi wote. Mkakati utatumika kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu zoezi la Sensa na utawezesha kuchukuliwa kwa hatua za pamoja za kutatua changamoto na matatizo yatakayojitokeza wakati wa mchakato wa Uelimishaji na Uhamasishaji.

Kama chombo cha uhamasishaji wa jamii na utafutaji rasilimali, Mkakati umelenga kushawishi wananchi, wadau wa maendeleo, jumuiya ya wafanyabiashara, asasi za kiraia na wadau wengine, kuhakikisha kuwa kuna ushiriki na mchango mzuri katika utekelezaji wa zoezi la Sensa. Mkakati unajielekeza katika kuelimisha na kuhamasisha kama njia yenye ufanisi ya kutoa taarifa za masuala muhimu katika hatua za kabla ya kuhesabu watu, wakati wa kuhesabu watu na baada ya kuhesabu watu, ambazo ufanisi wake unaweza kufikiwa kwa kuweka mazingira wezeshi kwa watekelezaji wakuu na wadau. Kwa hiyo, shughuli za uhamasishaji wa Sensa katika Mkakati huu zimekusudia kuwafanya wadau wote kupata uelewa na kuzingatia masuala yanayohusu zoezi zima la Sensa.

Kupitia shughuli za uelimishaji, jamii itakuwa na uelewa kamili juu ya umuhimu wa mchakato wa Sensa, uelewa kuhusu madodoso ya Sensa na maswali yaliyomo kwenye madodoso na utayari wa kujibu maswali kwa ufasaha hivyo kupata takwimu bora za Sensa. Upatikanaji wa takwimu bora za Sensa utaongeza matumizi ya takwimu katika kupanga mipango, kufanya maamuzi, na matumizi mengine ya kuleta maendeleo ya Taifa. Kwa upande mwingine, shughuli za uhamasishaji wa Sensa zinajielekeza katika kuweka msingi wa kisheria, kutafuta uungwaji mkono na kupata dhamira thabiti ya viongozi katika ngazi zote, na ukusanyaji wa rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa Sensa.

Kwa hiyo, Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji umelenga kuchangia kufikiwa kwa malengo ya Sensa, ambayo ni kuongeza upatikanaji wa takwimu bora na zinazoaminika, kila wakati, kuhusu kuongezeka kwa idadi ya watu na mwelekeo sahihi wa viashiria vya kiuchumi na kijamii. Aidha, Mkakati utaongeza uelewa wa wadau kuhusu takwimu za kijamii, kiuchumi, idadi ya watu na mwenendo wa ongezeko la watu nchini Tanzania. Zaidi ya hayo, Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji utawezesha kuongezeka kwa matumizi ya taarifa za kidemografia, kijamii kiuchumi na mazingirazilizochambuliwa kitaalamu. Pia, utaimarisha uwezo wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar katika kutekeleza Sensa ya Watu na Makazi, hasa katika kupanga, kukusanya, kuchakata, kuchambua, kusambaza, kutumia takwimu za Sensa na katika kufanya tafiti mbalimbali.

Mchakato wa utayarishaji wa Mkakati huu ulizingatia uzoefu kutoka Sensa zilizopita za mwaka 2002 na 2012, ripoti za methodolojia za Sensa za Mwaka 2002 na 2012, ripoti za utafiti wa kutathmini Sensa za Watu na Makazi za Mwaka 2002 na 2012 pamoja  na Kitabu cha Utekelezaji na Usimamizi wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022. Aidha, Mkakati ulizingatia uzoefu uliopatikana katika kazi za tafiti mbalimbali za kitakwimu zilizofanyika katika kipindi cha kati ya Sensa ya mwaka 2012 hadi 2021.

Uandaaji wa Mkakati huu pia ulizingatia uzoefu kutoka katika baadhi ya nchi zilizofanya Sensa za Watu na Makazi katika mzunguko wa Umoja wa Mataifa wa kufanya Sensa ya Watu na Makazi katika miaka ya 2020 (The United Nations 2020 Round of Population and Housing Census). Mzunguko huu wa Umoja wa Mataifa unaanzia mwaka 2015 hadi 2024. Vilevile, maandalizi hayo yalizingatia hali ya mabadiliko makubwa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano yalivyosaidia utekelezaji wa shughuli za kitakwimu ikiwemo Sensa ya Mwaka 2022, ambayo itahitaji matumizi zaidi ya teknolojia mpya kuliko ilivyokuwa katika Sensa zilizopita.

Mkakati huu wa Uelimishaji na Uhamasishaji una sura tisa. Sura ya Kwanza ina sehemu mbili ambazo ni utangulizi mfupi kuhusu Sensa zilizofanyika nchini; na maelezo ya mchakato uliotumika katika kuandaa mkakati huu. Sura ya Pili inaelezea uchambuzi wa masuala na uzoefu uliopatikana kutokana na Sensa zilizopita ambao unasaidia kuboresha utekelezaji wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022. Sura ya Tatu inaelezea malengo ya Uelimishaji na Uhamasishaji na matokeo yake ambayo Mkakati unalenga kuyapata katika awamu zote tatu za Sensa. Sura ya Nne inachambua wadau wa Sensa wakati Sura ya Tano inaelezea mikakati na shughuli kubwa za kufikia matokeo yanayotarajiwa.

Sura ya Sita inaelezea juu ya utayarishaji wa jumbe na nyenzo za uhamasishaji, wakati Sura ya Saba inaelezea muundo wa kitaasisi wa Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji ili kuwezesha utekelezaji wa Mkakati. Sura ya Nane na ya Tisa zinaelezea juu ya mpango kazi wa Sensa kwa miaka minne (2020/2021-2023/24) na mfumo wa ufuatiliaji na tathmini mtawalia.

# YALIYOMO


**SHUKRANI** ........ **II**

**DIBAJI** ........ **III**

**YALIYOMO** ........ **V**

**SURA YA KWANZA** ........ **7**

UTANGULIZI ........ 7

***1. Utangulizi*** ........ *7*

***2. Usuli*** ........ *7*

***3. Umuhimu wa Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji*** ........ *8*

***4. Uelimishaji na Uhamasishaji*** ........ *8*

***5. Uelimishaji kuhusu Sensa*** ........ *8*

***6. Uhamasishaji wa Sensa*** ........ *9*

**SURA YA PILI** ........ **10**

UCHAMBUZI WA MASUALA YA SENSA KWA AJILI YA UELIMISHAJI NA UHAMASISHAJI ........ 10

***1. Utangulizi*** ........ *10*

**SURA YA TATU** ........ **21**

MALENGO NA MATOKEO YA MKAKATI WA UELIMISHAJI NA UHAMASISHAJI WA SENSA YA MWAKA 2022 ........ 21

***1. Lengo Kuu la Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022*** ........ *21*

***2. Malengo Mahsusi ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022*** ........ *22*

***3. Malengo ya Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji*** ........ *22*

***4. Matokeo ya Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji wa Sensa*** ........ *23*

***5. Kabla ya Kuhesabu Watu*** ........ *23*

***6. Wakati wa Kuhesabu Watu*** ........ *24*

***7. Baada ya Kuhesabu Watu*** ........ *24*

**SURA YA NNE** ........ **25**

UCHAMBUZI WA WALENGWA ........ 25

***1. Utangulizi*** ........ *25*

***2. Wafanya Maamuzi*** ........ *26*

***3. Watekelezaji*** ........ *26*

***4. Wanufaika*** ........ *27*

***5. Wadau wa Utafutaji wa Rasilimali*** ........ *27*

**SURA YA TANO** ........ **28**

MIKAKATI MAHSUSI NA SHUGHULI ZAKE ........ 28

***1. Utangulizi*** ........ *28*

***2. Mikakati ya Uelimishaji na Uhamasishaji na Matokeo yake*** ........ *28*

***3. Mikakati na Kazi zitakazofanyika Kabla ya Kuhesabu Watu*** ........ *28*

***4. Kuongezeka kwa Uelewa wa Jamii kuhusu Sensa*** ........ *29*

***Kuongezeka kwa rasilimali kutoka Jumuiya ya Wafanyabiashara na Asasi za Kiraia*** ........ *30*

*Kuimarisha Uwezo wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar kutekeleza Mkakati huu* ..... 30
*Mikakati na Kazi Zitakazofanyika Wakati wa Kuhesabu Watu* ..... 31
*Kuimarika kwa Uelewa wa Jamii kuhusu Sensa* ..... 31

**SURA YA SITA** ..... **34**

KUANDAA MAUDHUI NA NJIA ZA KUPELEKA UJUMBE ..... 34
*1. Utangulizi* ..... 34
*2. Uandaaji wa Maudhui* ..... 34
*3. Utayarishaji wa Nyenzo za Uhamasishaji wa Sensa* ..... 35
*4. Uchaguzi wa Njia za Mawasiliano* ..... 35

**SURA YA SABA** ..... **45**

MUUNDO WA KITAASISI WA MKAKATI WA UELIMISHAJI NA UHAMASISHAJI WA SENSA 2022 ..... 45
*1. Utangulizi* ..... 45
*2. Uratibu na Usimamizi wa Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji* ..... 45
*3. Uratibu na Taratibu za Usimamizi wa utekelezaji wa Mkakati* ..... 45
*4. Majukumu na Wajibu wa Kamati* ..... 47
*5. Kitengo cha Uelimishaji na Uhamasishaji* ..... 47
*6. Kamati ya Kitaifa ya Uhamasishaji wa Sensa* ..... 47
*7. Kamati za Uhamasishaji za Mikoa na Wilaya* ..... 48
*8. Kamati za Uhamasishaji wa Sensa za Serikali ya Mtaa na Shehia* ..... 50
*9. Chama cha Wabunge wa Tanzania Juu ya Masuala ya Watu na Maendeleo* ..... 50
*10. Kikosi Kazi cha Uelimishaji na Uhamasishaji* ..... 51

**SURA YA NANE** ..... **53**

MPANGO KAZI WA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA MKAKATI WA UELIMISHAJI NA UHAMASISHAJI WA SENSA ..... 53
*1. Utangulizi* ..... 53

**SURA YA TISA** ..... **62**

UFUATILIAJI NA TATHMINI YA MKAKATI WA UELIMISHAJI NA UHAMASISHAJI ..... 62
*1. Utangulizi* ..... 62
*2. Ratiba ya Shughuli za Uelimishaji na Uhamasishaji* ..... 62
*3. Kabla ya Kuhesabu Watu* ..... 62
*4. Wakati wa Kuhesabu Watu* ..... 62
*5. Baada ya Kuhesabu Watu* ..... 62
*6. Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini* ..... 63
*7. Mpango wa Uwasilishaji wa Taarifa* ..... 66
*8. Mfumo wa Uwasilishaji wa Taarifa kwa Wadau wa Ndani* ..... 66
*9. Uwasilishaji wa Taarifa ya Utekelezaji kwa Wadau wa Nje* ..... 67

**ORODHA YA REJEA** ..... **68**

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1. Utangulizi

Sura hii inaeleza kwa kifupi Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022. Aidha, inagusia historia ya Sensa nchini, changamoto na uzoefu uliopatikana; masuala ya mbinu na matumizi ya teknolojia. Sura hii pia inaeleza umuhimu wa kuwa na Mkakati huu.

### 2. Usuli

Tanzania itafanya Sensa ya sita ya Watu na Makazi mwezi Agosti, 2022. Sensa nyingine tano zilizotangulia, zilifanyika katika miaka ya 1967, 1978, 1988, 2002 na 2012.

Madhumuni ya Sensa ya Watu na Makazi ni kusaidia upatikanaji wa takwimu sahihi zilizochambuliwa, ili kuandaa na kutekeleza Sera, kufuatilia na kutathmini mipango na programu za maendeleo katika ngazi ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Sensa inatoa takwimu za kidemografia, kijamii na kiuchumi ambao ndio msingi wa maandalizi ya sera za kiuchumi na kijamii. Takwimu hizi pia hutumika kufuatilia kuimarika kwa ubora wa hali za maisha ya wananchi.

Aidha, takwimu za Sensa ya Mwaka 2022 zitasaidia kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26); Dira ya Maendeleo 2025; Dira ya Zanzibar 2050; Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano Zanzibar (2021/22- 2025/26); Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030) na Ajenda ya Afrika 2063. Matokeo ya Sensa ya Mwaka 2022 yatatumika pia katika kutayarisha Dira mpya ya Maendeleo ya Tanzania Bara.

Tofauti na Sensa zilizopita, Sensa ya mwaka 2022 pia itakusanya taarifa za majengo yote yalipo nchini bila kujali aina ya matumizi na itachukua taarifa za anuani za makazi. Takwimu za majengo zitasaidia kuandaa Sera ya nyumba na kupata takwimu za umasikini usio wa kipato. Anwani za Makazi zitasaidia kurahisisha upatikanaji, utoaji na ufikishaji wa huduma mbalimbali kwa wananchi hasa kwenye biashara mtandao.

Sensa ya Watu na Makazi ni zoezi linalohitaji ushiriki na ushirikiano wa kila mdau na wananchi. Ili kupata ushiriki na ushirikiano huo, kila mdau ni lazima aelimishwe vya kutosha kuhusu Sensa, aelewe madhumuni na faida za Sensa, na zaidi ya hayo, kuwepo na ufahamu wa kutosha wa majukumu ya wadau katika kufanikisha Sensa. Hivyo, Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji ni sehemu ya mchakato wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, ambao lengo lake kuu ni kuweka mazingira wezeshi katika ngazi ya Taifa, Mkoa, Wilaya hadi ngazi ya chini ya utawala ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa zoezi la Sensa.

## 3. Umuhimu wa Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji

Mafanikio ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 yatapimwa kwa ubora wa takwimu zitakazokusanywa. Mafanikio haya yatapatikana iwapo taarifa zitakazokusanywa ni sahihi, kamilifu na zinazokubalika na wadau. Haya yatawezekana iwapo wadau na umma kwa ujumla, watakuwa na ufahamu na wataunga mkono ipasavyo zoezi la Sensa. Kwahiyo, jitihada za pamoja lazima zichukuliwe kuelimisha na kuhamasisha wadau kuhusu umuhimu wa Sensa na jukumu lao katika kuifanikisha. Kwa mantiki hiyo, Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji una nafasi ya pekee katika kufanikisha Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022. Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji (2022), unalenga kutatua changamoto zilizojitokeza katika Sensa zilizopita, hususani, za mwaka 2002 na 2012. Kwa ajili hiyo, ni muhimu kuwa na kampeni iliyoandaliwa na kuratibiwa vyema ili kuelimisha, kuhamasisha na kutangaza mchakato wa Sensa.

## 4. Uelimishaji na Uhamasishaji

Uelimishaji na Uhamasishaji ni mbinu za mawasiliano zenye malengo, mikakati na matokeo anuai. Wakati uelimishaji unalenga kujenga uelewa na ufahamu kwa jamii kuhusu jambo fulani, kupata uungwaji mkono, na kuongeza ushiriki wa wanajamii katika kampeni au jambo jingine lolote; uhamasishaji unahusu hatua zinazolenga kufanikisha uungwaji mkono katika kutekeleza jambo fulani. Uhamasishaji pia unajenga mazingira wezeshi ambayo yanajumuisha upatikanaji wa rasilimali. Kampeni za uelimishaji na uhamasishaji kwa pamoja zinaleta ushirikishwaji mpana wa wadau katika kufikia malengo yaliyokusudiwa.

## 5. Uelimishaji kuhusu Sensa

Katika Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 shughuli za uelimishaji zitafanyika kwa kutumia mbinu mbalimbali ambazo zitahusisha taarifa za kwenye radio na runinga, magazeti, mitandao ya kijamii, matamasha ya michezo, muziki, mikutano ya hadhara, warsha na mijadala katika ngazi zote.

Matokeo yanayokusudiwa ni kuongeza uelewa wa umma na ushiriki wake katika hatua zote za utekelezaji wa Sensa. Zaidi ya hayo, uelimishaji unatarajiwa kupunguza au kuondoa dhana na imani potofu dhidi ya Sensa na kupunguza au kuondoa makosa katika kujibu maswali katika dodoso. Mkazo mahsusi utawekwa katika kuonesha thamani na umuhimu wa Sensa kwa Taifa na kwa mwananchi mmoja mmoja, katika kupanga mipango ya maendeleo katika maeneo yao, na hususan, katika utoaji wa huduma kwa jamii, kama huduma za elimu, afya, maji, nishati na rasilimali nyingine.

Watakaohusika katika kazi za uelimishaji watakuwa viongozi wa kitaifa, Makamisaa wa Sensa, viongozi wa Asasi za Kiraia na Makundi ya Kitaaluma, Viongozi wa dini, Viongozi wa vyama vya siasa, Maafisa wa Sensa, Kamati za Sensa za Mikoa, Wilaya na Kata/Shehia/Kitongoji, Vyombo vya Habari na Maafisa Uhusiano, watu mashuhuri, wasanii, wanamichezo, makarani na wasimamizi wa Sensa.

## 6. Uhamasishaji wa Sensa

Miongoni mwa mbinu zitakazotumika katika kuhamasisha Sensa ni mikutano itakayohusisha viongozi wakuu, mashauriano, mijadala ya kitaifa, matukio ya kitaifa na mikutano na wadau. Matokeo yanayotarajiwa ni kupata ushiriki wa umma kwa ukamilifu na hatimaye kuongeza kiwango cha kuungwa mkono na kupata misaada ya utaalamu na rasilimali fedha kwa shughuli mbalimbali za Sensa, kuwa na muundo wa Sensa unaofanya kazi na kuwapo mazingira wezeshi na endelevu ya kufanyia Sensa.

Wahusika wakuu katika uhamasishaji wa Sensa ni viongozi wa kitaifa, Makamisaa wa Sensa, Kamati Kuu ya Sensa, Kamati ya Taifa ya Uhamasishaji, Kamati ya Wataalamu ya Sensa, Kamati za Sensa za Mikoa, Wilaya na Kata/Shehia/Kitongoji. Wengine ni Wadau wa Maendeleo, Wataalamu kutoka Taasisi za Elimu ya Juu na Taasisi za Kitafiti na Taasisi za Kitaaluma.




Viongozi wa Kisiasa, Kidini na Kimila wa ngazi zote wana jukumu kubwa la kufanikisha Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022. Pichani, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akinyanyua Usinga kuwasalimia wananchi mara baada ya kusimikwa kuwa Mkuu wa Machifu wote Tanzania na kuitwa jina la Hangaya lenye maana ya Nyota inayong`aa, katika Tamasha la Utamaduni la 'Mila na Desturi zetu' lililofanyika katika Viwanja vya Redcross Kisesa Magu, Mkoani Mwanza (Picha na Maktaba).

# SURA YA PILI

## UCHAMBUZI WA MASUALA YA SENSA KWA AJILI YA UELIMISHAJI NA UHAMASISHAJI

### 1. Utangulizi

Sura hii inachambua changamoto na mambo yaliyojitokeza katika Sensa zilizopita ambayo yamezingatiwa katika kuandaa Mkakati huu wa Uelimishaji na Uhamasishaji wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.

Masuala yaliyojitokeza katika Sensa zilizopita yaliyoathiri utekelezaji wa mchakato wa Sensa yamebainishwa kama ifuatavyo:

i. Kushindwa kuhamasisha uungwaji mkono stahiki, ushirikiano na ushiriki wa wadau wakiwamo Jumuiya ya Wafanyabishara/Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia. Hii ilitokana na kutowashirikisha kabisa au kutowashirikisha kwa wakati muafaka. Uchambuzi wa Sensa ya mwaka 2012 unaonesha kuwa wadau hawa hawakushirikishwa ipasavyo hivyo kutopata michango yao.
ii. Mchakato wa Sensa kuhusishwa na siasa; hili ni tatizo ambalo ukubwa wake hauwezi kupimwa kirahisi. Lakini katika baadhi ya maeneo ushabiki wa kisiasa ulishamiri na kusababisha hofu miongoni mwa wananchi na hivyo kusababisha ushiriki duni.
iii. Baadhi ya mila na imani za kidini zilitumika kuwavunja moyo wananchi kushiriki Sensa, jambo hili halina budi kuangaliwa kwa umakini.
iv. Baadhi ya viongozi hawakuwa na utayari wa kuunga mkono shughuli za Sensa katika awamu zote tatu za mchakato wa Sensa (Kabla ya Kuhesabu Watu, Wakati wa ya Kuhesabu Watu na Baada ya Kuhesabu Watu). Hii inaelezwa ilitokana na kutokuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu umuhimu na faida za Sensa.
v. Kutokana na ukubwa wa gharama za uendeshaji wa zoezi la Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 na matumizi ya teknolojia ya kidijitali katika Sensa ya mwaka 2022, ina maanisha kuwa wadau wengi zaidi wanahitajika kushiriki kugharamia zoezi hilo.

**Jedwali Na. 2.1: Masuala na Changamoto za Sensa Kabla ya Kuhesabu Watu**

| Tukio | Tatizo /Changamoto | Chanzo /Sababu | Walengwa | Hatua za uhamasishaji na uelimishaji zinazohitajika |
|---|---|---|---|---|
| 1.Bajeti na Ufadhili | Upungufu wa fedha | ▪ Gharama kubwa za Sensa,<br>▪ Uchache wa rasilimali za Serikali<br>▪ Serikali kukabiliwa na vipaumbele vingi vya kuvigharamia | ▪ Wizara ya Fedha na Mipango, Tanzania Bara na Zanzibar<br>▪ Kamati Kuu ya Sensa<br>▪ Makamisaa wa Sensa | Kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali za kutosha |

| Tukio | Tatizo /Changamoto | Chanzo /Sababu | Walengwa | Hatua za uhamasishaji na uelimishaji zinazohitajika |
|---|---|---|---|---|
| | Utaalamu | ▪ Upungufu wa utaalamu na vifaa | ▪ Wizara ya Fedha na Mipango, Tanzania Bara na Zanzibar<br>▪ Utumishi, Tanzania Bara na Zanzibar<br>▪ Kamati Kuu ya Sensa<br>▪ Makamisaa wa Sensa | Kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali za kutosha na kujengea watumishi uwezo |
| | Kutotumika vya kutosha kwa vyanzo vya rasilimali rasmi na visivyo rasmi | - Uelewa mdogo juu ya Sensa katika Sekta Binafsi na Asasi za Kijamii (AZAKI)<br>- Uhamasishaji hafifu wa vyanzo visivyo rasmi vya upatikanaji wa fedha<br>- Uhaba wa Msaada wa kitaalam | ▪ Wizara ya Fedha na Mipango, Tanzania Bara na Zanzibar<br>▪ Jumuiya ya Wafanyabiashara<br>▪ AZAKI | -Kuhamasisha kwa wakati unaofaa na kuziomba Sekta Binafsi na Asasi za Kijamii (AZAKI) kujitolea kutoa rasilimali na kushirikiana katika shughuli za Sensa.<br>-Kuhamasisha sera za kupanua wigo wa vyanzo vya kodi |
| | Uungwaji mkono hafifu kutoka kwa Wadau wa Maendeleo | -Kuwapo kwa programu nyingi zinazohitaji fedha.<br>-Ushirikishwaji mdogo | - Wadau wa Maendeleo<br>-Mashirika ya Kimataifa | Kuhamasisha Wadau wa Maendeleo kupitia majukwaa mbalimbali ili kuongeza misaada na rasilimali zinazohitajika. |
| 2. Utengaji maeneo | -Uchache wa Ramani/ramani zilizopitwa na wakati<br>- Baadhi ya maeneo ya mjini kutumia picha za satelaiti<br>- Uhaba wa ramani; baadhi ya maeneo ya mjini hayakuwa na ramani kubwa<br>- Uhaba wa usafiri kwa watendaji wa kazi za kutenga maeneo | - Kukosekana kwa fedha za kutosha<br>- Ukosefu wa utaalamu<br>- Gharama kubwa za Teknolojia mpya | -Kamati Kuu ya Sensa<br>- Viongozi wa Serikali za Mitaa<br>- Kamati ya Wataalamu wa Sensa<br>- Wataalamu wa Sensa<br>- Mamlaka za Mikoa na Wilaya | - Kutafuta ufadhili wa kugharamia utayarishaji wa picha za satelaiti na usafirishaji wa vifaa.<br>- Matumizi ya teknolojia ya kisasa. |

| Tukio | Tatizo /Changamoto | Chanzo /Sababu | Walengwa | Hatua za uhamasishaji na uelimishaji zinazohitajika |
|---|---|---|---|---|
| 3.Matayarisho ya Dodoso | -Kuchelewa kukamilishwa kwa dodoso<br><br>-Ucheleweshaji wa usambazaji wa madodoso katika maeneo ya kuhesabia | - Kushirikishwa wadau kwa wakati<br>- Usambazaji wa Madodoso kwa wakati | - Kamati ya wataalam wa Sensa<br>- Wizara ya Fedha na Mipango Tanzania Bara na Zanzibar,<br>- Wizara,<br>- Idara<br>- Mashirika na Wadau wengine<br>- Kamati ya Vifaa | - Kuendesha mkutano wa watumiaji wa taarifa za Sensa ili kujadili yaliyomo katika Dodoso la Sensa<br>- Kuzingatia Mpango Kazi wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.<br>- Kuwahamasisha viongozi wa kitaifa kuhusu maswali yaliyomo katika Dodoso la Sensa.<br>- -Kuendesha kampeni kusaidia upatikanaji wa ushuiriki bora wa Jamii. |
| 4.Sensa ya Majaribio | -Kukataa kuhesabiwa | - Uelewa mdogo wa baadhi ya wanajamii kuhusu madhumuni na faida ya takwimu zitokanazo na Sensa<br>- Imani potofu dhidi ya kuhesabiwa<br>- Kiwango kisichotosheleza cha utoaji wa taarifa za Sensa wa vyombo vya habari<br>- Uhamasishaji usiotosheleza wa Sensa ya Majaribio | - Viongozi wa Serikali<br>- Viongozi wa Jumuiya za Kiraia, dini na Serikali za Mitaa<br>- Wanajamii katika maeneo ya yanayoendeshwa Sensa ya Majaribio<br>- Watendaji Wakuu wa Vyombo vya Habari | - Kuelimisha jamii kuhusu madhumuni ya Sensa na faida ya takwimu zitokanazo na Sensa<br>- Kusambaza kijitabu cha ufafanuzi wa maswali ya Sensa na kitabu cha maelezo ya msingi kuhusu Sensa ya Watu na Makazi<br>- Kufanya kampeni ili kupata ushirikiano bora wa jamii<br>- Kuhamasisha Watendaji wakuu wa Vyombo vya Habari kuboresha taarifa zao<br>- Kushirikishwa viongozi wenye ushawishi na viongozi wa dini |
| | Kuwepo uingiliaji na ghiliba za kisiasa | - Dhana ya kunufaika kisiasa | - Wanasiasa | - Kuwahamasisha Wanasiasa |
| | Msaada wa vifaa usiotosheleza | - Upungufu wa fedha<br>- Uhaba wa usafiri na wafanyakazi | - Wizara ya Fedha na Mipango, Tanzania Bara na Zanzibar | - Kuhamasisha ugawaji bora wa rasimali<br>- Kuhamasisha ushirikishwaji wa |

| Tukio | Tatizo /Changamoto | Chanzo /Sababu | Walengwa | Hatua za uhamasishaji na uelimishaji zinazohitajika |
|---|---|---|---|---|
| | | | - Kamati Kuu ya Sensa<br>- Makamisaa wa Sensa<br>- Sekta Binafsi/AZAKI<br>- Washirika wa Maendeleo | washirika wa maendeleo katika upatikanaji wa rasimali |
| 5. Uajiri na mafunzo ya Makarani na Wasimamizi | -Uhaba wa makarani na wasimamizi wenye sifa katika baadhi ya maeneo<br>- Muda mfupi wa mafunzo kwa vitendo | - Kutozingatiwa kwa vigezo vya uajiri<br>-kukosekana kwa ushirikiano na baadhi ya taasisi za serikali<br>- Uhaba wa fedha za mafunzo ya wasimamizi na makarani wa kuhesabu | - Viongozi wa kisiasa,<br>- Wafanyakazi wa Sensa<br>- Viongozi wa Mikoa na Wilaya<br>- Watendaji wakuu wa wizara, Idara na Taasisi zake.<br>- Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Takwimu<br>- Wataalamu wa Sensa<br>- Wizara ya Fedha na Mipango, Tanzania Bara na Zanzibar<br>- Viongozi wa Kijamii | - Kutoa matangazo ya ajira ya makarani wa Sensa na wasimamizi<br>- Kutoa taarifa sahihi na za kutosha kwa watendaji wa vyombo vya habari juu ya ajira za makarani wa Sensa.<br>- Kushawishi upatikanaji wa rasilimali zaidi kwa mafunzo ya makarani wa Sensa na wasimamizi.<br>- Mipango sahihi na uratibu mzuri wa mafunzo ya Sensa<br>- Kutolewa mafunzo ya kutosha juu ya matumizi ya vifaa vya kukusanyia taarifa.<br>- |

## Jedwali Na. 2.2: Masuala na Changamoto za Sensa Wakati wa Kuhesabu Watu

| Tukio | Tatizo/changamoto | Chanzo/sababu | Walengwa | Shughuli za Uhamasishaji |
|---|---|---|---|---|
| 6. Kuhesabiwa | -Imani na mitazamo kuhusu kuhesabiwa | - Ukosefu wa elimu sahihi ya Sensa<br>-Kutawaliwa na imani za dini.<br>-Imani potofu | -Viongozi wenye ushawishi na wanaosikilizwa na jamii<br>-Vyombo vya Habari<br>-Jamii<br>-Viongozi wa dini | -Kuendesha mikutano ya uhamasishaji kwa viongozi wa dini, wenye ushawishi na wanaosikilizwa na jamii<br>-Kuhamasisha jamii kushirikiana na |

| Tukio | Tatizo/changamoto | Chanzo/sababu | Walengwa | Shughuli za Uhamasishaji |
|---|---|---|---|---|
| | | | | makarani wa wa Sensa.<br>-Kutangaza kupitia vyombo vya habari maudhui ya Dodoso la Sensa. |
| | -Misimamo tofauti ya kisiasa<br>-Utangazaji na utoaji wa taarifa wa kiwango cha chini kuhusu masuala ya Sensa | -Ushirikiano hafifu kutoka kwa baadhi ya vyama vya siasa.<br>-Uhamasishaji dhaifu wa masuala ya Sensa | -Vyama vya Siasa<br>-Vyombo vya Habari | -Uhamasishaji wa viongozi wa siasa katika ngazi zote<br>-Kiwango cha juu cha ushiriki wa Vyombo vya habari kuhusu masuala ya Sensa ya watu na makaazi. |
| | -Kushindwa kuzifikia baadhi ya kaya hasa zilizo katika majengo yaliyofungwa na yaliyozungukwa na kuta ndefu | -Wasi wasi wa Usalama<br>-Uelewa mdogo | -Wakazi wa mjini na vitongoji vyake.<br>-Kamati Kuu ya Sensa<br>-Makamisaa wa Sensa | -Kutangaza njia na namna ya kuwatambua makarani na Wasimamizi wa Sensa<br>-Kutoa vitambulisho maalum kwa Makarani na Wasimamizi wa Sensa.<br>-Kuwashirikisha viongozi wa Serikali za mitaa katika maeneo husika. |
| | Usalama na ulinzi wa Makarani na Wasimamizi wa Sensa | -Dhana kuwa Makarani wa Sensa wana fedha<br>-Njia zisizo salama za usafiri katika baadhi ya maeneo<br>-Tabia za baadhi ya Makarani wa Sensa zinaweza kuwapotosha | -Vyombo vya Ulinzi na Usalama na Umma kwa ujumla<br>-Mamlaka za Serikali za Mitaa.<br>-Sekta Binafsi (wamiliki wa hoteli, na vyombo vya usafiri) | -Kuhamasisha ushirikiano wa vyombo vya ulinzi na usalama ili kulinda Makarani na Wasimamizi wa Sensa<br>-Kutoa elimu stahiki na kuelezea juu ya wajibu na |

| Tukio | Tatizo/changamoto | Chanzo/sababu | Walengwa | Shughuli za Uhamasishaji |
|---|---|---|---|---|
| | | watu kuwa wana pesa | | majukumu kwa wahusika wakuu<br>-Kuimarisha ushirikiano uliopo kati ya viongozi wa Serikali za mitaa na Makarani na Wasimamizi wa Sensa |
| | -Utoaji wa taarifa usiojitosheleza kuhusu masuala ya Sensa | -Ukosefu wa taarifa kamilifu juu ya maswala ya Sensa.<br>-Mpango Mkakati wa uelimishaji na uhamasishaji kushindwa kufika kwa ngazi za chini | -Kitengo cha Uhamasishaji katika Ofisi za Takwimu (NBS na OCGS)<br>-Vyombo vya Habari.<br>-Vikundi vya maigizo na wahamasishaji | -Kutangaza siku ya Sensa.<br>-Kuhamasisha upatikanaji rasilimali ili kuviwezesha vyombo vya habari kuitangaza Sensa kwa ufanisi<br>-Mafunzo stahiki kwa wanahabari. |
| 7.Hoja zinazohusiana na udadisi | -Kutokufikiwa kwa baadhi ya maeneo ya kuhesabia watu | -Utengaji wa maeneo ya kuhesabia watu usiokamilifu<br>-Mgawanyo usio sahihi wa kazi kwa Makarani wa Sensa<br>-Mabadiliko ya makadirio ya ukubwa wa maeneo ya kuhesabu watu hasa katika maeneo ambayo yamejengwa makazi mapya.<br>-Upungufu wa vyombo vya usafiri.<br>-Mabadiliko ya idadi ya kaya katika baadhi ya | -Kitengo cha GIS kwa upande wa NBS/OCGS<br>-Wasimamizi na Makarani wa Sensa<br>-Viongozi wa jamii | -Kuongeza umakini katika kutenga maeneo ya kuhesabia watu<br>-Kutoa ufafanuzi sahihi wa majukumu na wajibu wa Makarani wa Sensa na Wasimamizi.<br>- Kuhamasisha viongozi wa kijamii juu ya haja ya kushirikiana na Makarani wa Sensa.<br>-Kufanya mapitio na Kusahihisha maeneo ya kuhesabu watu |

| Tukio | Tatizo/changamoto | Chanzo/sababu | Walengwa | Shughuli za Uhamasishaji |
|---|---|---|---|---|
| | | maeneo ya kuhesabia watu.<br>-Majanga ya kiasili katika baadhi ya maeneo. | | kabla ya zoezi la kuhesabu.<br>-Kuimarisha usimamizi wakati wa Sensa |
| | -Kukiukwa kwa taratibu za uajiri kwa Wasimamizi na Makarani wa Sensa. | -Kutokufuatwa kwa Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake<br>-Taratibu za uteuzi wa Wasimamizi na Makarani wa Sensa hazikutekelezwa kwa uwazi. | -Ofisi za NBS na OCGS<br>-Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar.<br>-TAMISEMI<br>-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>-UTUMISHI | -Kuuhamasisha uongozi wa NBS na OCGS kuandaa maelezo ya taratibu na viwango vya uajiri.<br>-Kuzihamasisha na kuzishirikisha Kamati za Mikoa na Wilaya<br>- Kuepusha upendeleo katika mchakato wa uteuzi wa Makarani na Wasimamizi wa Sensa.<br>-Kuanzisha Kanzidata ya Makarani wa Sensa na Wasimamizi. |

| Tukio | Tatizo/changamoto | Chanzo/sababu | Walengwa | Shughuli za Uhamasishaji |
|---|---|---|---|---|
| | - Siku saba za kuhesabu hazikutosheleza katika maeneo ambayo yalihesabiwa kwa kutumia Dodoso Refu | -Ukubwa wa Dodoso refu<br>-Uteuzi usio sahihi wa Wasimamizi na Makarani wa Sensa | -Kamati ya wataalamu<br>-Wadau wa takwimu | -Kudhibiti wingi wa maswali katika dodoso<br>-Kuwekwa Mkazo wa kuelimisha umma juu ya maudhui ya Dodoso la Sensa |
| | -Kuwepo kwa Changamoto ya baadhi ya jamii kutofahamu vyema lugha ya Kiswahili. | -Kukosa elimu rasmi ya msingi<br>-Tabia ya kuhamahama kwa baadhi ya jamii<br>-Utaratibu wa mila na tamaduni | -Kamati za Sensa za Mikoa na Wilaya.<br>-Ofisi za NBS na OCGS<br>-Wizara za Elimu<br>-Viongozi wa dini/mila/wenye ushawishi kwenye jamii | -Kuainisha maeneo yenye watu wasiofahamu Kiswahili<br>-Kuajiri Makarani na Wasimamizi wa Sensa ambao wanafahamu lugha za maeneo husika<br>-Kuweka utaratibu wa kutoa elimu dhidi ya mila potofu. |
| | -Baadhi ya akinamama kutoruhusiwa na waume zao kujibu baadhi ya maswali wanayoulizwa | -Taratibu za mila na tamaduni<br>-Nafasi ya jinsia kwa mtazamo wa mila | -Wazee na viongozi wenye ushawishi | -Kuhamasisha ushiriki wa pamoja katika ngazi ya kaya.<br>-Kuboresha elimu kwa Umma kupitia Vyombo vya Habari |
| | -Baadhi ya maswali na majibu kuhitaji ufafanuzi na kuandikwa upya | -Mafunzo yasiyojitosheleza kwa wasimamizi na Makarani wa Sensa | -Kamati ya Wataalamu ya Sensa | - Kusambaza kijitabu cha ufafanuzi wa maswali ya Sensa na kitabu cha maelezo ya msingi kuhusu Sensa ya Watu na Makazi |
| | -Kushindwa kutoa majibu kwa maswali yanayohusu umiliki wa mali | -Kulihusisha zoezi la Sensa | -Kamati za Sensa za | -Kuongeza ufahamu na uhamasishaji |

| Tukio | Tatizo/changamoto | Chanzo/sababu | Walengwa | Shughuli za Uhamasishaji |
|---|---|---|---|---|
| | | na masuala ya kutozwa kodi.<br>-Imani za kijadi | Mikoa na Wilaya<br>-Viongozi wa jadi<br>-Watu wenye ushawishi katika jamii | juu ya malengo ya Sensa. |
| | -Ugumu wa kuwafikia watu ambao wanaishi katika maeneo ya mbali:<br>-Kufikisha Wasimamizi, Makarani na Vifaa vya Sensa | -Miundombinu mibovu | -Ofisi za Sensa NBS na OCGS na Wizara za Fedha na Mipango (Tanzania Bara na Zanzibar) | -Kuandaa vyombo sahihi vya usafiri (magari, boti, ndege, treni, pikipiki)<br>-Makarani na Wasimamizi watoke kwenye maeneo husika |
| 8. Usimamizi | -Ushirikiano hafifu wa baadhi ya viongozi wa Mikoa, Wilaya na Serikali za Mitaa | -Uelewa mdogo juu ya umuhimu wa Sensa | -Kamati za Sensa za Mikoa na Wilaya.<br>-Mamlaka za Serikali za Mitaa.<br>-Ofisi za NBS na OCGS. | -Kuelimisha na kuhamasisha<br>Viongozi wa Mikoa, Wilaya na Mamlaka za Serikali za Mitaa |
| | -Usimamizi usiotosheleza | -Msimamizi mmoja kupangiwa Makarani wengi na maeneo makubwa ya kuhesabia<br>-Rasimali chache za kuwezesha uajiri wa Wasimamizi wakutosha. | -Kamati Kuu ya Sensa<br>-Kamati ya wataalamu ya Sensa.<br>-Ofisi za OCGS na NBS | -Kutenga rasilimali na vifaa vya kutosha<br>-Kuajiri Wasimamizi wa kutosha wa zoezi la Sensa |

### Jedwali Na. 2.3: Masuala na Changamoto za Sensa Baada ya Kuhesabu Watu

| Tukio | Tatizo/changamoto | Chanzo/sababu | Walengwa | Uelimishaji na Uhamasishaji |
|---|---|---|---|---|
| 9. Utafiti Baada ya Kuhesabu Watu | -Kiwango kidogo cha taarifa zilizotolewa kupitia vyombo vya habari baada ya utafiti | -Upatikanaji usiotosheleza wa taarifa za sensa kwa vyombo vya habari<br>- Upya wa zoezi la Utafiti wa baada ya Sensa | -Ofisi za NBS na OCGS<br>-Vyombo vya Habari<br>-Serikali katika ngazi ya Wilaya, Serikali za Mitaa | -Kuelimisha kuhusu umuhimu wa Utafiti wa baada ya Sensa<br>-Kutayarisha mikutano na vyombo vya habari na kutoa taarifa kwa watendaji wa vyombo vya habari.<br>-Kuhamasisha jamii kutoa taarifa sahihi |
| | -Hesabu ya idadi ya watu iliyopandishwa na kushushwa, (nakala ya taarifa za Sensa). | -Mtazamo juu ya faida za Sensa kijamii na kiuchumi zinazopatikana<br>-Uelewa mdogo wa taarifa za utafiti baada ya Sensa | - Ofisi za NBS na OCGS<br>-Wanasiasa na Viongozi wa Serikali za Mitaa | -Kujenga uelewa juu ya umuhimu na malengo ya utafiti wa baada ya Sensa<br>-Kusambaza taarifa za matokeo ya Thathmini na Ufuatiliaji ya matokeo ya Sensa. |
| | | -Mitazamo ya faida za kijamii na kiuchumi zinazopatikana | -Viongozi wa Serikali za Mitaa<br>-Wanasiasa<br>-Sekretarieti ya Ofisi ya Sensa | -Kuwa na uangalizi wa karibu<br>-Kuwahamasisha viongozi wa Serikali za Mitaa na wa kimila juu ya umuhimu wa taarifa sahihi za Sensa. |
| 10. Mchakato na uchambuzi wa taarifa | -Ucheleweshaji wa uchambuzi na utolewaji wa taarifa za Sensa<br>-Matumizi hafifu ya taarifa za Sensa | -Kukosekana kwa umeme wa uhakika.<br>-Uchaguzi usio sahihi wa teknolojia<br>-Uchambuzi wa awali wa madodoso kutoka katika maeneo ya Sensa<br>-Kutokuwahusisha watumiaji wa | -Ofisi za Takwimu za NBS, OCGS<br>-Wadau wa Maendeleo<br>-Makarani na Wasimamizi wa Sensa.<br>-Watumiaji wa data wakiwemo Wadau wa Maendeleo.<br>-Mawakala wa masoko | -Kuhamasisha misaada ya kifedha na utaalamu.<br>-Kununuliwa jenereta za dharura kwa wakati.<br>-Kuandaa Mafunzo kwa Makarani wa Sensa na kuendesha mikutano ya watumiaji wa taarifa za Sensa kama vile Taasisi za serikali, Sekta binafsi, Azaki na Taasisi za Kimataifa.<br>-Kuingiza taarifa mara kwa mara kwenye mtandao kurahisisha huduma kwa watumiaji. |

| Tukio | Tatizo/changamoto | Chanzo/sababu | Walengwa | Uelimishaji na Uhamasishaji |
|---|---|---|---|---|
| | | mwisho wa taarifa za Sensa.<br>-Kukosekana kwa mpango wa kutangaza na utumiaji wa taarifa za Sensa<br>-Ucheleweshaji wa usambazaji wa taarifa za Sensa | -Ofisi za Sensa (NBS, OCGS), Wizara, Idara na Mashirika yake. | -Kutayarisha machapisho maalumu ya Sensa katika magazeti yenye wasomaji wengi<br>-Kuandaa majarida yenye taarifa za Sensa na kuyasambaza nchi nzima. |

# SURA YA TATU

## MALENGO NA MATOKEO YA MKAKATI WA UELIMISHAJI NA UHAMASISHAJI WA SENSA YA MWAKA 2022

### 1. Lengo Kuu la Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022

Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji wa Sensa unadhamiria kufanikisha malengo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022. Lengo kuu ni kupata takwimu sahihi zitakazotumika kupanga mipango ya maendeleo, kutunga Sera, kutoa huduma za jamii pamoja na kuwezesha ufuatiliaji na tathmini ya programu za maendeleo.

Aidha, Mkakati huu unalenga kujenga ushirikishwaji wa jamii na kuandaa mazingira mazuri katika awamu zote tatu za utekelezaji wa Sensa kupitia shughuli mbalimbali, kuanzia ngazi ya Taifa hadi ngazi ya Kitongoji/Mtaa/Shehia. Shughuli hizi zitafanyika kwa njia mbalimbali ikiwemo matumizi ya vyombo vya habari.

Kwa kuzingatia gharama kubwa za kuendesha zoezi la Sensa, Mkakati umeandaliwa ili kuhamasisha wadau wa Maendeleo, Jumuiya ya Wafanyabiashara na Asasi za Kiraia katika kuchangia rasilimali za kuendesha zoezi la Sensa.





Mikutano ya hadhara kama hii pichani sio tu inarahisisha utoaji wa elimu ya Sensa kwa wananchi bali inawafanya kujiamini kwa kuwa inatoa fursa ya kuuliza maswali na kuondoa wasiwasi juu ya baadhi ya mambo ambayo hawayafahamu hivyo kupelekea kujibu maswali kwa usahihi wakati Karani wa Sensa anapofika katika kaya siku ya Sensa (Picha na Maktaba). Kushoto ni Kamisaa wa Sensa Tanznaia Bara Mhe. Anne Makinda na Kulia ni Kamisaa wa Sensa Tanzania Zanzibar Balozi Mohamedi Haji Hamza

## 2. Malengo Mahsusi ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022

Malengo mahsusi ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 ni kama yafuatayo:

i. Kuongeza upatikanaji wa takwimu sahihi za kidemografia, kijamii na kiuchumi kwa wakati na zinazoaminika;
ii. Kuongeza uelewa wa wadau kuhusu hali ya kijamii, kiuchumi na kidemografia ya wananchi wa Tanzania pamoja na aina na mwenendo wa ukuaji wake;
iii. Kuongeza utumiaji wa takwimu zilizochambuliwa za kijamii, kiuchumi na kidemografia;
iv. Kuimarisha uwezo wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar wa kutekeleza Sensa ya Watu na Makazi hasa katika kupanga, kukusanya, kuchakata, kuchambua, kusambaza na kutumia takwimu rasmi za Sensa na takwimu nyingine.

## 3. Malengo ya Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji

Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji unalenga kufanikisha malengo ya jumla ya Sensa katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2024. Mkakati una malengo makuu matatu, na kila lengo lina malengo yake mahsusi.

i. Kuelimisha na kuhamasisha wadau wote ili kupata uungwaji mkono na ushirikiano wa kutosha.

   **Malengo Mahsusi**
   - Kushirikisha Asasi za Kiraia na jamii kwa jumla katika utekelezaji wa Sensa kwenye ngazi zote.
   - Kuongeza ushiriki wa Viongozi wa Jamii, Wabunge, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Asasi za Kiraia katika kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa Sensa.

ii. Kuhamasisha kukubalika kwa Takwimu za Sensa na kuongeza matumizi yake kwa watumiaji mbalimbali.

   **Malengo Mahususi**
   - Kutumia njia mbalimbali kusambaza takwimu za Sensa;
   - Kuandaa machapisho ya matokeo ya Sensa ambayo ni rahisi kueleweka kwa watumiaji;
   - Kuimarisha urahisi wa kupata Takwimu za Sensa katika tovuti za NBS na OCGS; na
   - Kuunganisha tovuti za NBS, OCGS na za wadau wa Takwimu

iii. Kuhakikisha ushirikiano endelevu na wa uhakika wa Serikali na viongozi wake katika ngazi zote, Wadau wa Maendeleo na Jumuiya ya Wafanyabiashara ili ziwepo rasilimali za kutosha na kuhakikisha watu wote watakaokuwapo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania usiku wa Kuamkia Siku ya Sensa, wanahesabiwa.

**Malengo mahsusi**

- Kutoa taarifa mara kwa mara za hali ya utekelezaji wa zoezi la Sensa;
- Kushirikisha wadau katika matukio muhimu ya Sensa;
- Kuandaa na kusimamia akaunti maalumu za mitandao ya kijamii ili kuwafikia wadau wa Sensa

## 4. Matokeo ya Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji wa Sensa

Malengo ya Mkakati yanatarajiwa kutoa matokeo yafuatayo:

i. Kuongezeka uelewa kwa Asasi za Kiraia, jamii kwa ujumla kuhusu umuhimu wa Sensa katika ngazi zote;
ii. Kuongezeka kwa ushiriki na uungwaji mkono wa viongozi wa Asasi za Kiraia na jamii kwa jumla;
iii. Kuongezeka kwa wigo wa uelimishaji na uhamasishaji wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022;
iv. Kuongezeka kwa uelewa wa jamii juu ya umuhimu wa Sensa;
v. Uwepo wa uungwaji mkono endelevu na utashi wa Serikali, Watunga Sera, Wadau wa Maendeleo, Jumuiya ya Wafanyabiashara na Asasi za Kiraia katika zoezi la Sensa;
vi. Kuimarishwa kwa ushirikiano endelevu na vyombo vya habari; na
vii. Kuongezeka kwa kiwango cha usambazaji na matumizi ya takwimu za Sensa kwa watumiaji mbalimbali.

Kwa jumla, Mkakati umelenga kuweka mazingira wezeshi na rafiki ya kutekeleza zoezi la Sensa katika awamu zake zote tatu. Hivyo, shughuli za uelimishaji na uhamasishaji wa Sensa katika awamu hizo tatu zitakuwa kama ifuatavyo:

## 5. Kabla ya Kuhesabu Watu

Shughuli za Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji zitajikita katika kukuza uelewa wa jamii kuhusu Sensa ya Majaribio kupitia kampeni kwenye vyombo vya habari na njia nyingine za mawasiliano. Katika awamu hii, jitihada zaidi zitaelekezwa kwenye uelimishaji na uhamasishaji kwa ajili ya kuungwa mkono na wadau wa maendeleo na jamii. Wadau wa Maendeleo wataombwa kusaidia rasilimali ili kuziba pengo katika bajeti ya Sensa. Aidha, Jumuiya ya Wafanyabiashara, vyombo vya habari na Asasi za Kiraia zitaombwa kujitolea kufanikisha zoezi la Sensa kupitia bajeti zao za shughuli za kijamii. Katika awamu hii, Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar zitajengewa uwezo ili kufanikisha utekelezaji wa Mkakati huu.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na Makamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 Mhe. Anne Makinda na Balozi Mohamed Haji Hamza ofisini kwake Ikulu Zanzibar (Picha na Maktaba).

## 6. Wakati wa Kuhesabu Watu

Awamu ya Kuhesabu Watu italenga zaidi katika kuwaandaa wananchi kutoa ushirikiano kamilifu katika zoezi la kuhesabu watu. Hivyo, Mkakati huu utaweka mkazo mkubwa katika kuondoa hofu na mawazo potofu kuhusu zoezi la Sensa ili kujenga utayari wa kuhesabiwa.



Rais Jakaya Kikwete akiwakaribisha makarani wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012 walipofika kwenye makazi yake Ikulu kwa ajili ya kuhesabiwa (Picha na Maktaba).

Mkakati utatumia njia mbalimbali kuifikia jamii ambayo inatakiwa kutoa taarifa sahihi kwa mujibu wa madodoso ya Sensa na kutekeleza matakwa mengine yatakayojitokeza. Taarifa zitakazokusanywa zitakuwa ni za siri na zitatumika kwa masuala ya kitakwimu tu na si vinginevyo.

## 7. Baada ya Kuhesabu Watu

Katika awamu hii ya Sensa, kazi zitakazofanyika ni kufanya tathmini, kusambaza matokeo na kuhimiza matumizi ya takwimu. Lengo la tathmini ni kuangalia uhalisia na ubora wa matokeo ya Sensa. Hivyo, katika kipindi hiki Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji utalenga katika kuwaelewesha wadau mbalimbali kuhusu uwepo wa takwimu za Sensa na namna ya kuzipata ili kuhamasisha kufanya maamuzi kwa kufuata taarifa sahihi za kitakwimu.




Viongozi wa ngazi zote wana jukumu kubwa la kufanikisha Sensa ya Watu na Makazi. Picha hii inamuonesha Rais wa Jamhuri wa Tanzania Jakaya Mrisho Kikwete akiambatana na viongozi wengine wa kitaifa wakiwa na nyuso za furaha mara baada ya Rais Kikwete kuzindua matokeo ya Sensa ya

# SURA YA NNE

## UCHAMBUZI WA WALENGWA

### 1. Utangulizi

Shughuli za Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji wa Sensa zinakusudia kuwafikia walengwa mbalimbali ambao ni mtu mmoja mmoja, watunga sera, viongozi katika ngazi mbalimbali na umma kwa ujumla.

Makundi haya ya walengwa ni muhimu kuyaainisha katika Mkakati huu ili kupima ufahamu wao kuhusu Sensa, masuala yanayowahusu, kitu gani kinawavutia, na mengineyo. Kwa hiyo, uchambuzi wa kina wa wadau mbalimbali lazima ufanyike ili kutambua mbinu tofauti ambazo Mkakati huu utazitumia kufikia malengo yake. Uchambuzi wa kina wa wadau unalenga kuhakikisha mkakati unafikia malengo yanayopimika. Kwa muktadha huo, ni muhimu kuainisha aina ya wadau na mahitaji yao ya taarifa za Sensa.

Dhana ya wadau katika mkakati huu ina maana sawa na dhana ya walengwa au kundi maalumu la wadau kwa ajili ya uenezaji wa taarifa na uhamasishaji. Uchambuzi umeainisha aina tatu ya wadau yaani Wafanya Maamuzi, Watekelezaji na Wanufaika.

Kwa mantiki hiyo, walengwa ni pamoja na watu binafsi, makundi ya watu au taasisi zenye uwezo wa kufanya maamuzi au kushawishi watu kufanya maamuzi mahsusi na kuchukua hatua kuhusu sera na rasilimali, ikiwemo fedha na utekelezaji wa masuala ya Sensa. Katika kuchambua walengwa husika, vigezo vifuatavyo vilitumika na vitaendelea kutumika katika kila hatua:

i. Kiwango cha uelewa wa masuala ya Sensa;
ii. Kiwango anachoonesha katika kusaidia/kushiriki Sensa;
iii. Maslahi yake katika Sensa; na
iv. Faida inayotarajiwa kwa mlengwa wa Sensa.

Yafuatayo ni maelezo ya makundi matatu ya wadau yaliyoainishwa katika Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji wa Sensa:

## 2. Wafanya Maamuzi

Kundi hili ni wale wanaoshiriki katika mchakato wa kufanya maamuzi, uratibu na usimamizi katika zoezi la Sensa, yaani:

i. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
ii. Rais wa Zanzibar;
iii. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
iv. Makamu wa Pili wa Rais (Zanzibar);
v. Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi;
vi. Mawaziri na Maofisa Waandamizi wa Serikali;
vii. Makamisaa wa Sensa;
viii. Wafanyakazi wa Asasi za Kiraia;
ix. Sekretarieti ya Sensa;
x. Vitengo vya Habari (NBS & OCGS);
xi. Timu ya Uelimishaji na Uhamasishaji wa Sensa; na
xii. Kamati za Sensa Taifa, Mkoa na Wilaya.

Kwa kuwa wajibu wa wadau hawa ni kuhakikisha kwamba Sensa inafanyika kwa ufanisi, na matokeo ya kuaminika yanapatikana kwa wakati, watahusishwa katika kuhamasisha na kuelekeza hatua zitakazoleta uungwaji mkono katika jitihada za uelimishaji na uhamasishaji.

Mbinu kuu za uelimishaji na uhamasishaji kwa kundi la Wafanya Maamuzi zitakuwa ni Majadiliano, Mijadala, Makubaliano na Ushawishi.

## 3. Watekelezaji

Walengwa hawa ni ambao mara nyingi wanashawishi Wafanya Maamuzi kuchukua hatua. Hawa wana jukumu la kuhakikisha maamuzi ya kuwezesha utekelezaji wa zoezi la Sensa yanafanyika kulingana na kalenda ya Sensa.

Hawa ni pamoja na:

i. Wizara husika;
ii. Wamiliki na Wafanyakazi wa Vyombo vya Habari;
iii. Viongozi wa Mikoa na Wilaya;
iv. Wadau wa Maendeleo;
v. Asasi za Kiraia, Taasisi za Kitaaluma, Taasisi za Elimu ya Juu na Utafiti;
vi. Viongozi wa Kimila; na
vii. Viongozi wa Dini.

Kundi hili la wadau limepewa umuhimu mkubwa katika kazi za uelimishaji na uhamasishaji. Aidha, kundi hili litahamasishwa na kuwezeshwa kutekeleza mikakati na kazi za kuelimisha na kuhamasisha katika ngazi ya Taifa hadi ya Wilaya. Kwa

mantiki hiyo, watawajibika kuhakikisha utekelezaji mzuri wa zoezi la Sensa kupitia msaada wa utaalamu na fedha.

Mbinu kuu za uelimishaji; uhamasishaji kwa kundi la Watekelezaji zitakuwa ni majadiliano, mijadala, makubaliano, ushawishi na mafunzo ya kujenga uwezo.

### 4. Wanufaika

Kundi hili linaundwa na watumiaji wa takwimu za Sensa ambao uungaji mkono na ushiriki wao ni muhimu katika mafanikio ya zoezi la Sensa. Wanufaika hawa wana haki ya kudai upatikanaji wa takwimu zilizo sahihi za Sensa. Ni muhimu kundi hili kuelimishwa ili lidai kuwapo kwa mchakato sahihi wa Sensa na matokeo yanayokubalika: Kundi hili linajumuisha:

i. Wizara, Idara na Wakala wa Serikali;
ii. Wadau wa Maendeleo;
iii. Wanasiasa;
iv. Makundi ya Dini;
v. Asasi za Kiraia, Taasisi za Kitaaluma, Taasisi za Elimu ya Juu na Utafiti;
vi. Jumuiya ya Wafanyabiashara; na
vii. Umma.

Mbinu kuu za uelimishaji; Uhamasishaji kwa kundi la wanufaika zitakuwa majadiliano, kuhamasisha, makubaliano na ushawishi.

Kwa ujumla, uchambuzi uliofanywa kuhusu wadau mbalimbali umebainisha kuwa tayari kuna uelewa wa wastani hadi wa juu na dhamira ya kusaidia utekelezaji wa Sensa miongoni mwa makundi ya walengwa, hasa walengwa wanaofanya maamuzi na utekelezaji, kwani wengi wao wanashiriki katika mfumo wa Takwimu wa Taifa.

### 5. Wadau wa Utafutaji wa Rasilimali

Kwa kawaida zoezi la Sensa lina gharama kubwa na linahitaji rasilimali nyingi. Mkakati huu umeainisha baadhi ya wadau muhimu katika uhamasishaji wa upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya kutekeleza zoezi la Sensa ya mwaka 2022. Hivyo, mkakati huu umeainisha wadau muhimu wafuatao katika jitihada za utafutaji wa rasilimali.

i. Wadau wa Maendeleo;
ii. Jumuiya ya Wafanyabiashara na Asasi za Kiraia; na
iii. Wamiliki na mameneja wa vyombo vya habari.

Mbinu mbalimbali za uhamasishaji zitatumika kutafuta uungwaji mkono wa wadau katika utekelezaji wa zoezi la Sensa. Mbinu hizi ni pamoja na ushawishi, ushirikishaji, majadiliano, makubaliano, mijadala na uwezeshaji. Kila kundi la wadau wa Sensa lililoainishwa litahamasishwa kupeleka ujumbe wa Sensa kwenye maeneo yao.

# SURA YA TANO

## MIKAKATI MAHSUSI NA SHUGHULI ZAKE

### 1. Utangulizi

Mikakati mahsusi na shughuli zinazohusiana na uelimishaji na uhamasishaji wa Sensa vinakwenda sambamba na zoezi la Sensa ili kuhakikisha kuna muunganiko kati ya Mkakati huu na mikakati mingine. Hii itaimarisha utekelezaji wa Sensa na matumizi ya takwimu zitokanazo na Sensa.

### 2. Mikakati ya Uelimishaji na Uhamasishaji na Matokeo yake

Ili kuweka mazingira mazuri na wezeshi kwa ajili ya kufanya Sensa, mikakati kadhaa imeainishwa. Mikakati hiyo ni kama ifuatavyo:

i. Kushirikisha Wabunge, Viongozi wa Dini, Asasi za Kiraia, Jumuiya za wanataaluma, Taasisi za Elimu ya Juu na Utafiti na Jamii katika ngazi zote;
ii. Kujenga Ushirikiano na Jumuiya ya Wafanyabiashara;
iii. Kuimarisha Ushirikiano na Vyombo vya Habari na Wakuu wa Taasisi;
iv. Kukuza Majadiliano na Mijadala kuhusu Sensa;
v. Kuwahusisha na kuwashirikisha wadau muhimu wakiwamo Wadau wa Maendeleo;
vi. Kuwajengea uwezo maofisa wa Sensa na kamati za Sensa katika ngazi zote; na
vii. Kuimarisha utafutaji na ufuatiliaji wa Rasilimali.

Mikakati hii itatumika kupata matokeo katika kila awamu ya utekelezaji wa Sensa.

### 3. Mikakati na Kazi zitakazofanyika Kabla ya Kuhesabu Watu

Katika hatua ya maandalizi, msisitizo wa msukumo wa Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji na shughuli zake utakuwa kwenye kusaidia mipango na menejimenti ya Sensa.

Mipango hii itahusu utafutaji fedha na misaada mingine ya hali na mali kutoka kwa wadau wote wakiwemo wa makundi ya Jumuiya za Wafanyabiashara na Asasi za Kiraia. Mambo muhimu yanayopaswa kufanyika ili kujenga msingi imara wa kuendesha Sensa, ni elimu na uhamasishaji wa jamiii kuhusu taratibu za Sensa. Aidha, uimarishaji wa uwezo wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar unahitajika ili kusimamia uetekelezaji wa Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji. Kazi za Sensa zitafanyika kutoka ngazi ya kitaifa hadi ngazi ya Kitongoji/Mtaa/Shehia. Matokeo muhimu (yanayotarajiwa) katika awamu hii ni:

i. Kuongezeka kwa uelewa wa jamii kuhusu zoezi la Sensa;
ii. Kuongezeka kwa rasilimali kutoka kwa wadau wakiwamo Wafanyabiashara na Asasi za Kiraia; na
iii. Kuimarishwa kwa uwezo wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar ili ziweze kutekeleza mkakati huu.

## 4. Kuongezeka kwa Uelewa wa Jamii kuhusu Sensa

Mkakati mkuu 1: Ushirikiano na vyombo vya habari na Asasi za Kiraia.

**Kazi katika Ngazi ya Kitaifa:**

i. Kuandaa mikutano ya mashauriano na wamiliki wa vyombo vya habari na mameneja wao kujadili uenezaji, uelimishaji na uhamasishaji wa habari za Sensa;
ii. Kutoa elimu kwa wahariri na waandishi wa habari kuhusu zoezi la Sensa, mchakato na matokeo yake;
iii. Kusaidia uandaaji wa vipindi vya habari ili kutoa elimu kwa jamii kuhusu Sensa vyenye lengo la kujenga uelewa kuhusu Sensa;
iv. Kusaidia kikosi kazi cha waandishi wa habari na maofisa uhusiano ili kutoa elimu ya Sensa kupitia vyombo vya Habari;
v. Kutayarisha vifaa vya uelimishaji na uhamasishjai wa Sensa; na
vi. Kuandaa taratibu za usambazishaji wa Takwimu za Sensa.



Vyombo vya Habari ni wadau wakubwa katika kufanikisha Sensa ya Watu na Makazi. Pichani kundi la wapiga picha wakichukua picha za kumbukumbu za familia ya Rais Kikwete (Haipo pichani) ilipohesabiwa katika Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012 Ikulu Dar es Salaam (Picha na maktaba).

**Ngazi ya Mkoa na Wilaya:**

i. Kuhamasisha vyombo vya habari kutoa elimu kwa umma kuhusu Sensa; na
ii. Kuviwezesha vyombo vya habari kushirikiana na Kamati za Sensa za Mikoa na Wilaya.

***Mkakati mkuu 2: Uhamasishaji wa Asasi za Kiraia na Baadhi ya Taasisi***

**Kazi katika ngazi ya Kitaifa:**

i. Kufanya mikutano na Asasi za Kiraia za kitaifa kuhusu mchakato wa Sensa;
ii. Kuwezeshwa kuanzishwa muungano wa makundi ya kutoa elimu ya Sensa;
iii. Kuimarisha uwezo wa Asasi muhimu za Kiraia kuhusu Sensa na umuhimu wake;

iv. Kuandaa semina kwa ajili ya Asasi za Kiraia, Taasisi za Kitaaluma, Taasisi za Elimu ya Juu na Utafiti kuhusu faida za Sensa kiuchumi na kijamii;

v. Kuandaa mashindano kuhusu Sensa kwa wanafunzi wa shule, vyuo na vyuo vikuu;

vi. Kutoa taarifa za mara kwa mara kwa viongozi wa kitaifa kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa Sensa; na

vii. Kuimarisha ushirikiano na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mawaziri na wakuu wa vyombo vya habari kwa ajili ya ushiriki katika zoezi la Sensa.

**Ngazi ya Mkoa na Wilaya:**

i. Kuandaa warsha kwa Asasi za Kiraia kuhusu Sensa;

ii. Kuziwezesha Asasi za Kiraia kuandaa mikutano kwa umma kuhusu Sensa na madodoso ya Sensa;

iii. Kuziwezesha Kamati za Sensa za Mikoa na Wilaya kufanya kazi na Asasi za Kiraia ili kuwezesha kupatikana kirahisi kwa taarifa za Sensa; na

iv. Kuandaa mashindano ya uhamasishaji wa Sensa kwa kushindanisha Mikoa, Wilaya na Kitongoji, Mtaa/Shehia.

**Kuongezeka kwa rasilimali kutoka Jumuiya ya Wafanyabiashara na Asasi za Kiraia**

***Mkakati mkuu 1: Kujenga ushirikiano na Jumuiya ya Wafanyabiashara na Asasi za Kiraia***

**Kazi katika ngazi ya Kitaifa:**

i. Kuandaa mikutano ya kushauriana na wadau wakuu wakiwemo Jumuiya ya Wafanyabiashara na Asasi za Kiraia kuhusu Sensa na mahitaji ya rasilimali;

ii. Kuandaa mikutano ya ushirikiano, kujadiliana na kuongeza uelewa wa Jumuiya ya Wafanyabiashara na Asasi za Kiraia kuhusu Sensa na manufaa yake; na

iii. Kuandaa timu ya pamoja ya kufuatilia upatikanaji wa rasilimali na matumizi yake.

**Kuimarisha Uwezo wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar kutekeleza Mkakati huu**

***Mkakati mkuu 1: Kujenga uwezo wa Ofisi za Takwimu katika utoaji habari na mbinu za uhamasishaji***

**Kazi katika ngazi ya Kitaifa:**

i. Kuandaa mafunzo ya uhamasishaji kwa vitengo vya uelimishaji na uhamasishaji vya Ofisi za Takwimu na kikosi kazi cha uhamasishaji;

ii. Kuwezesha mikutano ya kitaifa, Kamati za Sensa za Mkoa na Wilaya kuhusu uelimishaji na uhamasishaji wa sensa;

iii. Kuunda timu ya pamoja ya Ofisi za Takwimu na Jumuiya ya Wafanyabiashara/Vyombo vya habari /Asasi za Kiraia ili kuwa na uratibu bora wa uelimishaji, uhamasishaji na ufuatiliaji wa Sensa; na

iv. Kuunda timu ya kuratibu utengenezaji wa maudhui na nyenzo za uelimishaji na uhamasishaji wa Sensa.

**Mikakati na Kazi Zitakazofanyika Wakati wa Kuhesabu Watu**

Kwenye awamu hii, ndipo zoezi la kuhesabu watu linapofanyika na wananchi wanatarajiwa kuwajibika kufuata taratibu za Sensa kwa kushiriki kwa ukamilifu katika kujibu maswali. Uzoefu unaonesha kwamba malengo ya zoezi la Sensa huleta hofu na wasiwasi kwa baadhi ya watu wanaohojiwa. Kwa hiyo, mkazo utawekwa zaidi katika kuhakikisha kulinda usiri wa taarifa zinazokusanywa, na kwamba maelezo yatatolewa ya kuwa taarifa zinazokusanywa ni kwa ajili ya matumizi ya kitakwimu tu. Mikakati na mbinu mbalimbali zitatumika kuwaaminisha wananchi kwamba taarifa zinazokusanywa kwenye madodoso ya Sensa ni muhimu katika kupanga mipango ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Kwa hiyo, mikakati ya uhamasishaji itatumika kuanzia ngazi ya Taifa hadi Kitongoji/Mtaa/Shehia.

**Kuimarika kwa Uelewa wa Jamii kuhusu Sensa**

***Mkakati mkuu 1: Uandaaji wa vifaa vya ujumbe***

**Kazi katika ngazi ya Kitaifa:**

i. Kuandaa ujumbe na vifaa vya elimu kwa umma kama mabango, t-shirt, kofia, khanga, vitenge, skafu, tai, stika, matangazo, vijarida, video na *infographics* kwenye mitandao ya kijamii;

ii. Usambazaji wa vifaa vya ujumbe wa uhamasishaji kupitia vyombo vya habari na njia mbalimbali za mawasiliano katika ngazi ya jamii; na

iii. Kuratibu mrejesho wa ujumbe wa Sensa.

**Ngazi ya Mkoa na Wilaya:**

i. Kuandaa matamasha ya utamaduni ili kuielimisha jamii kuhusu Sensa;

ii. Kusambaza maudhui ya Sensa kwa ajili ya matumizi ya kwenye vyombo vya habari vya kieletroniki, magazeti na mitandao ya kijamii;

iii. Kuimarisha uwezo wa Kamati za Sensa za Mikoa na Wilaya; na

iv. Kuwawezesha wajumbe wa Kamati za Sensa za Mikoa na Wilaya kufanya mikutano ya kuielimisha jamii kuhusu Sensa

***Mkakati mkuu 2: Uhamasishaji wa Asasi za Kiraia, Taasisi za Kitaaluma, Elimu ya Juu na Utafiti***

**Kazi katika ngazi ya Taifa:**
Kuwezesha Asasi za Kiraia, Taasisi za Kitaaluma, za Elimu ya Juu na za Utafiti kufanya mijadala ya kitaifa kuhusu Sensa.

**Ngazi ya Mkoa na Wilaya**

i. Kutoa mafunzo kwa Asasi za Kiraia kuelewa madodoso ya Sensa na ukusanyaji wa taarifa; na

ii. Kuwezesha Asasi za Kiraia kuandaa mikutano ya wananchi kuhusu mchakato wa Sensa.

**Mikakati na Kazi zitakazofanyika Baada ya Kuhesabu Watu**

**Mikakati na Shughuli Husika**

Sensa ya Watu na Makazi ni chanzo kikuu cha taarifa kwa sababu inazalisha takwimu ambazo kama zikitumiwa ipasavyo, zinasaidia matumizi yenye tija ya rasilimali za Taifa. Kwa maana hiyo, mkakati huu utajikita katika kuhamasisha na kuzishawishi taasisi mbalimbali na wadau wakuu kuwezesha kupatikana kwa takwimu za Sensa ambazo ni sahihi na zinazoaminika zitakazozitumika katika kupanga mipango yao ya maendeleo.



Uelimishaji na Uhamasishaji wa Sensa ya Watu na Makazi unafanyika kwa njia nyingi ikiwemo kuwafikia wananchi katika maeneo yao hasa kwa jamii kama za wafugaji hawa (Pichani) ambao wako katika mazingira ambayo wakati mwingine ni vigumu kuwafikika (Picha na maktaba).

***Mkakati mkuu 1: Usambazaji wa takwimu za Sensa***

**Kazi katika ngazi ya Taifa:**

i. Kuandaa mkutano wa wadau ili kusambaza matokeo ya Sensa;

ii. Kuendesha mkutano wa kusambaza takwimu kwa walengwa;

iii. Kuandaa vipindi katika vyombo vya habari vinavyoelezea matokeo ya Sensa;

iv. Kutumia tovuti kuu ya Serikali, tovuti za Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine kusambaza matokeo ya Sensa; na

v. Kuandaa taarifa za matokeo ya Sensa katika mfumo rafiki kwa ajili ya watumiaji mbalimbali.

**Ngazi ya Mkoa na Wilaya:**

i. Kuandaa mikutano ya Asasi za Kiraia ili kusambaza taarifa mahsusi za Sensa katika ngazi ya Mkoa na Wilaya; na

ii. Kushirikisha vyombo vya habari vya ndani (magazeti na vya kielektroniki) katika kusambaza takwimu.

***Mkakati mkuu 2: Uandaaji Maudhui na Vifaa vya Uelimishaji na Uhamasishaji***

i. Kuwezesha uundwaji wa kikosi-kazi ili kuandaa maudhui ya matokeo ya Sensa kwa ajili ya walengwa mbalimbali;

ii. Kusambaza maudhui ya matokeo ya Sensa kwa wadau mbalimbali katika ngazi ya kitaifa hadi ngazi za Kitongoji/Mtaa/Shehia; na

iii. Kukusanya maudhui yatakayotokana na uchambuzi wa matokeo ya Sensa yatakayotumika katika kurekebisha mapungufu katika kupanga mipango ya maendeleo.

***Mkakati mkuu 3; Uelimishaji wa Wabunge, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Wizara, Idara na Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa***

i. Kuandaa vikao vinavyohusisha wabunge, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, madiwani, wizara, idara na wakala wa Serikali na mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuwaelimisha kuhusu takwimu za Sensa na matumizi yake katika kupanga mipango ya maendeleo; na

ii. Kuwaelimisha watumiaji wa takwimu za Sensa kutoka ngazi ya Taifa hadi ngazi ya Kitongoji/Mtaa/Shehia, kuhusu utumiaji wa Takwimu zilizopo katika kupanga mipango ya maendeleo.

# SURA YA SITA

## KUANDAA MAUDHUI NA NJIA ZA KUPELEKA UJUMBE

### 1. Utangulizi

Uandaaji wa maudhui kuhusu Sensa umepewa umuhimu mkubwa katika mkakati huu kutokana na ukweli kuwa watu hufanya maamuzi kutokana na taarifa wanazopata. Hivyo, maudhui yataandaliwa kulingana na aina ya kundi linalolengwa. Maudhui sahihi yatakayoweza kushawishi na kugusa mahitaji ya makundi mbalimbali ya walengwa yatasaidia makundi hayo kuwa na mtazamo chanya wa Sensa na hivyo kuwawezesha kushiriki kikamilifu.

### 2. Uandaaji wa Maudhui

Malengo makuu ya uandaaji wa maudhui ya kuelimisha na kuhamasisha umma kuhusu Sensa ni kufikisha ujumbe kwa walengwa. Aidha, mkakati huu utatumika kuwashawishi walengwa waunge mkono pamoja na kupata ushirikiano wao katika zoezi zima la Sensa.

Katika kuhakikisha utekelezaji wa Mkakati kwa ufanisi, kitaundwa kikosi kazi cha kutayarisha maudhui na nyenzo za uelimishaji na uhamasishaji katika ofisi za Takwimu (NBS na OCGS). Kwa kushirikiana na kamati ya utayarishaji wa maudhui na wataalamu wengine, kikosi kitahakikisha maudhui yanatayarishwa katika awamu zote tatu za Sensa.

Maudhui haya yataandaliwa kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

i. Ujumbe unaowasilishwa ubebe maana iliyokusudiwa;

ii. Lugha itakayotumika katika ujumbe iwe inafahamika na walengwa;

iii. Usahihi na mwendelezo wa utoaji ujumbe;

iv. Njia ya kutuma ujumbe/wabeba ujumbe;

v. Aina ya vyombo vitakavyotumika kuwasilisha ujumbe.

Mkakati umeandaliwa ili kuhakikisha ufanisi wa utoaji wa maudhui kwa kutumia muundo rahisi kwa walengwa unaozingatia:

i. Uainishaji wa masuala au changamoto husika katika awamu tatu za Sensa;

ii. Kufanya utafiti wa walengwa na uchambuzi wa wadau ili kujua uelewa, matakwa na utayari wao wa kuunga mkono ushiriki na uhamasishaji wa masuala ya Sensa;

iii. Kuandaa maudhui kwa kuzingatia uhalisia na uthibitisho;

iv. Kufanya tathmini ya awali ya maudhui kwa kupitia walengwa;

v. Kuboresha maudhui kwa kuzingatia maoni ya wadau;

vi. Kuandaa maudhui katika mfumo ambao ni rahisi kwa walengwa kuelewa; na

vii. Kuchagua njia ya mawasiliano inayofaa kupeleka ujumbe huo kwa walengwa.

### 3. Utayarishaji wa Nyenzo za Uhamasishaji wa Sensa

i Kama ilivyo kwa ujumbe, uandaaji wa nyenzo za uelimishaji na uhamasishaji umezingatia taratibu zifuatazo:

a. Matokeo ya utafiti kuhusu uelewa na mtazamo kuhusu Sensa;
b. Upimaji wa maswali na kufanya marekebisho ya dodoso;

ii Kutoa nyenzo zenye ubora na za kutosha kwa ajili ya kutumika kwenye vyombo vya habari na njia nyingine mbalimbali za mawasiliano.

iii Kutumia wataalamu miongoni mwa wadau kutayarisha na kuyawasilisha maudhui katika vyombo vya habari na njia nyingine za mawasiliano;

iv Kuanzisha mtandao mahsusi wa kusambaza ujumbe wa Sensa katika maeneo yasiofikika kiurahisi na ya pembezoni.

v Kutumia kamati za Sensa zinazoendelea na uelimishaji katika ngazi zote ili kuimarisha uhamasishaji;

vi Kulenga katika ujumbe mmoja mahsusi kwa kila kundi la walengwa husika au kuandaa vielelezo vinavyozingatia matakwa na mahitaji ya utamaduni na hali halisi ya Tanzania.

### 4. Uchaguzi wa Njia za Mawasiliano


Mafanikio ya ujumbe na nyenzo za mawasiliano za Sensa yanatokana na uchaguzi mzuri wa njia za mawasiliano na matumizi ya lugha rasmi pamoja na lugha ya alama. Uchaguzi wa njia za mawasiliano katika mkakati huu unaongozwa na vigezo vifuatavyo:

i. Aina ya makundi ya walengwa;

ii. Masuala na ujumbe wa uelimishaji na uhamasishaji wa Sensa; na

iii. Aina na mtindo wa kila chombo cha habari na njia ya mawasiliano.

Aina ya njia zitakazotumika zitabainishwa kulingana na ujumbe husika ulioandaliwa. Njia hizi zinajumuisha magazeti, vyombo vya kielekitroniki, mitandao ya kijamii, na njia za asili kama vile michezo ya kuigiza, mikutano, mashairi, na ngoma za jadi. Nyingine zitajumuisha taasisi kama Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Asasi za Kiraia na njia zisizo rasmi kwa kutumia viongozi wenye ushawishi kwa jamii.









Katika kuchagua njia ya mawasiliano Mkakati umezingatia aina ya walengwa ili kubaini njia sahihi ambayo itamwezesha mlengwa kufikiwa na ujumbe.

Baadhi ya mambo muhimu katika mchakato wa kuchagua njia za mawasiliano na makundi ya walengwa mkakati huu umezingatia:

i. Kufikia watu wengi au eneo kubwa kijiografia;
ii. Kuaminika na kutegemewa kwa njia zitakazopendekezwa;
iii. Idadi ya walengwa mahsusi;
iv. Njia ya mwasiliano inayopendwa na walengwa wengi;
v. Matumizi ya njia mchanganyiko;
vi. Njia muafaka kwa aina ya ujumbe unaokusudiwa kutolewa; na
vii. Gharama za kupeleka ujumbe kupitia njia hiyo.

Uandaaji wa ujumbe na uchaguaji wa njia unaainishwa katika Jedwali Na. 6.1

**Jedwali Na. 0.1: Utayarishaji wa Ujumbe na Njia za Kuufikisha**

| Tukio | Tatizo/ Changamoto | Mlengwa/ Mhusika | Maudhui ya Ujumbe | Njia ya mawasiliano | Hatua za Kuchukua |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. Bajeti na Ufadhili katika kugharamia zoezi la Sensa | - Uhaba wa fedha<br>- Gharama kubwa za Sensa<br>- Matumizi yasiyozingatia umuhimu wa kazi za Sensa<br>- Fedha kutolewa bila kuzingatia ratiba ya utekelezaji wa Sensa. | - Wizara ya Fedha na Mipango, Tanzania Bara na Zanzibar.<br>- Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi<br>- Kamati Kuu ya Sensa | - Uwekezaji katika programu za Sensa una faida kwa Mipango ya Maendeleo ya Taifa. | **Mtekelezaji:**<br>Mawaziri Wizara za Fedha na Mipango, Tanzania Bara na Zanzibar<br>- Makamisaa wa Sensa<br>**Njia:**<br>- Vikao vya bajeti katika Bunge na Baraza la Wawakilishi | - Kuhamasisha mgao wa kutosha wa rasilimali kulingana na mahitaji<br>- Kuwepo kwa ushawishi wa ngazi za juu wa uhamasishaji wa upatikanaji wa rasilimali za Sensa<br>- Mikakati ya uhamasishaji rasilimali kwa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022<br>- Kuweka udhibiti wa fedha za Sensa |
| | - Kukosekana kwa utaratibu na kuchelewa kutumia vyanzo visivyo rasmi vya rasilimali.<br>- Uelewa mdogo na kutokuwa na hamasa juu ya masuala ya Sensa kwa Jumuiya ya Wafanyabiashara na Asasi za Kiraia<br>- Uhamasishaji mdogo wa vyanzo rasmi vya fedha na msaada wa kitaalamu. | - Jumuiya ya Wafanyabiashara na Asasi za Kiraia | - Upatikanaji wa taarifa za Sensa unasaidia kufanya makadirio ya biashara na kukuza uwekezaji. | **Mjumbe:**<br>- Kamati Kuu ya Taifa ya Sensa na Mawaziri wenye dhamana ya fedha.<br>**Njia:**<br>- Mikutano ya Mashauriano na Vikao kati ya Makamisaa wa Sensa na Sekretarieti ya Sensa, na Asasi za kiraia na Jumuiya ya wafanyabiashara.<br>- Kutoa ripoti/ mrejesho wa matumizi ya rasilimali walizochangia | - Jumuiya ya Wafanyabiashara na Asasi za Kiraia kuchangia rasilimali katika zoezi la Sensa.<br>- Ushirikishaji wa mapema wa vyanzo visivyo rasmi vya rasilimali.<br>- -Kushirikisha kikamilifu Jumuiya ya Wafanyabiashara ili kukuza uelewa juu ya Sensa. |
| | -Uhamasishaji mdogo wa Wafadhili | - Wadau wa Maendeleo<br>- Mashirika ya Kimataifa | - Kuwekeza katika ukusanyaji, uchambuzi, utayarishaji na usambazaji wa taarifa za Sensa, | **Mjumbe:**<br>- Rais<br>- Makamu wa Rais<br>- Waziri Mkuu<br>- Makamu wa Pili wa Rais | - Wadau wa Maendeleo kutoa msaada wa kitaalamu na fedha. |

| Tukio | Tatizo/ Changamoto | Mlengwa/ Mhusika | Maudhui ya Ujumbe | Njia ya mawasiliano | Hatua za Kuchukua |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | huepusha upotevu wa rasilimali.<br>- Matokeo ya Sensa ni muhimu kwa mipango ya maendeleo, kuandaa sera na kufanya maamuzi sahihi. | - Mawaziri wa Fedha na Mipango<br>- Waziri wa Mambo ya Nje na Uhusiano wa Afrika Mashariki; na<br>- Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu<br>**Njia:**<br>- Mikutano ya mashauriano na makongamano<br>- Kutolewa ripoti kwa wadau wa maendeleo | |
| 2.Kuhamasisha ufanisi wa Kazi ya Kutenga maeneo | -Upungufu wa vyombo vya usafiri kwa wanaotenga maeneo ya kuhesabia watu<br>-Kuchelewa kufika kwa vifaa vya kutengea maeneo. | - Wizara ya Fedha na Mipango, Tanzania Bara na Zanzibar.<br>- Kamati ya Utaalam ya Sensa.<br>- Wataalamu wa kutenga maeneo<br>- Mamlaka za Mikoa na Wilaya | Kugharamia kazi za utengaji wa maeneo ni muhimu katika utekelezaji wa zoezi la Sensa | **Mjumbe:**<br>- Wizara ya Fedha na Mipango<br>- Ofisi ya Rais-Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>- Kamati ya uhamasishaji<br>**Njia:**<br>- Vikao<br>- Mikutano ya Mashauriano. | - Kutengwa fedha zaidi kwa kazi ya utayarishaji wa ramani za maeneo ikiwemo usafiri<br>- Ushirikiano toka kwa uongozi wa serikali za mitaa.<br>- Kuwasilishwa kwa wakati vifaa vya utengaji wa maeneo |
| 3. Maandalizi ya madodoso ya Sensa | -Kuchelewa kukamilishwa kwa madodoso | Kamati ya Wataalamu wa Sensa, Wizara, Idara na Wadau wengine | - Kuwasilishwa mapema kwa maoni kunawezesha kufanyika kwa Sensa ya Watu na Makazi kwa wakati.<br>- Dodoso lililoandaliwa vizuri linahakikisha ukusanyaji wa taarifa za Sensa zenye kiwango. | **Mjumbe:**<br>- Kamati ya Wataalam wa Sensa katika Ofisi za Sensa NBS na OCGS<br>**Njia:**<br>-Mikutano ya kupanga Sensa | - Kukamilishwa kwa dodoso la Sensa kwa mujibu wa Mpango kazi wa Sensa.<br>- Watumiaji wa taarifa za Sensa wapewe nafasi ya kutoa maoni yao kuhusu dodoso. |

| Tukio | Tatizo/ Changamoto | Mlengwa/ Mhusika | Maudhui ya Ujumbe | Njia ya mawasiliano | Hatua za Kuchukua |
|---|---|---|---|---|---|
| | - Taasisi husika za Sensa na wadau Kuchelewa kukamilisha na kuwasilisha maandalizi ya madodoso. | Watumiaji wa taarifa za Sensa na taasisi za Sensa | - wadau wakiwakilisha maoni yao mapema kutapelekea kufanyika kwa Sensa ya Watu na Makaazi kwa wakati.<br>- Dodoso lililotayarishwa vizuri linahakikisha upatikanaji na ubora wa data za Sensa | **Mjumbe:**<br>- Kamati ya wataalam wa Sensa katika ofisi za NBS na OCGS wadau<br>**Njia:**<br>Kuendesha mikutano ya watumiaji na wazalishaji wa takwimu za Sensa | - Wadau kushirikishwa na kukamilishwa kwa wakati utayarishaji wa madodoso<br>- Watumiaji wa taarifa za Sensa wapewe nafasi ya kutoa maoni yao kuhusu madodoso. |
| 4. Sensa ya Majaribio | - Kukataa kuhesabiwa<br>- Kiwango kisichoridhisha cha utolewaji wa habari za Sensa ya Majaribio kupitia vyombo vya habari<br>- Uhamasishaji mdogo wa Sensa ya Majaribio<br><br>-Kuchelewa kutumika kwa Teknolojia mpya | - Maofisa na Viongozi wa Serikali, viongozi wa dini, viongozi wenye ushawishi katika jamii<br>- Jamii katika maeneo yanayoendeshwa Sensa ya majaribio<br>- Wamiliki na Wahariri wa vyombo vya habari<br>- Ofisi za Sensa – NBS na OCGS<br>- Kamati ya wataalamu wa Sensa<br>- Wanahabari | - Ushiriki katika Sensa una faida ya upatikanaji wa huduma za kijamii na maisha bora<br>- Ushirikiano wa karibu kati ya kitengo cha Uelimishaji na Uhamasishaji na vyombo vya habari ni ufunguo wa mafanikio ya Sensa ya Majaribio<br>- Si vyema kutumia teknolojia mpya au utaratibu katika Sensa rasmi iwapo haujafanyiwa majaribio katika Sensa ya Majaribio<br>- Maswali yote ya Sensa lazima yafanyiwe majaribio katika Sensa ya Majaribio.<br>- Uwasilishaji wa maswali ya Sensa lazima unzingatie Mpango kazi wa Sensa ya | **Mjumbe:**<br>- Viongozi wa Serikali, viongozi wa dini, na viongozi wenye ushawishi katika jamii<br>**Njia:**<br>- Vyombo vya Habari vya kielektroniki, magazeti, mikutano ya hadhara, mkutano mahsusi<br><br>**Mjumbe**<br>- Ofisi za Sensa –NBS na OCGS, Kamati ya wataalamu ya Sensa<br>**Njia**<br>Mikutano ya kupanga Sensa | - Kuihamasisha Jamii ishirikiane na kushiriki kwa ukamilifu katika zoezi la Sensa.<br>- Kutoa taarifa za kina na za kutosha za uhamasishaji wa Sensa ya Majaribio.<br>- Kutumia teknolojia mpya ya kuchukulia na kuhifadhi taarifa kulingana na ratiba ya Sensa<br>- Matayarisho yafanyike kwa wakati unaofaa na uwasilishaji wa maswali ya Sensa uwe kulingana na ratiba ya Sensa. |

| Tukio | Tatizo/ Changamoto | Mlengwa/ Mhusika | Maudhui ya Ujumbe | Njia ya mawasiliano | Hatua za Kuchukua |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Watu na Makaazi. | | |
| | -Kujumuisha maswali yasiyofanyiwa majaribio katika Dodoso la Sensa. | Kamati Kuu ya Sensa, Kamati ya Ushauri ya Sensa na Kamati ya wataalamu ya Sensa. | marekebisho ya madodoso kulingana na matokeo ya Sensa ya majaribio | **Mjumbe**;<br>- Ofisi za Sensa (NBS na OCGS)<br>- Kamati Kuu ya Sensa.<br>- Kamati ya uhamasishaji<br><br>**Njia**<br>-Mkutano wa mashauriano na mwongozo Sensa | Kuandaa vikao vya kupitisha na kuidhinisha marekebisho ya madodoso |
| | -Kuchanganya mitazamo ya kisiasa na ghilba katika shughuli za Sensa | -Wanasiasa na Wabunge/ Wawakilishi<br>-Msajili wa Vyama vya Siasa.<br>-Kituo cha Demokrasia Tanzania.<br>-Wasomi<br>-Vyombo vya habari | - wasitumie majukwaa ya kisasa kuwapotosha wananchi kuhusu masuala ya Sensa | **Mjumbe:**<br>- Msajili wa Vyama vya Siasa.<br>- Kamati Kuu ya Sensa.<br>- Kamati ya wataalamu ya Sensa<br>**Njia**<br>- Mikutano<br>- Mazungumzo<br>- Mwongozo wa Sensa<br>- Vielelezo vya Uhamasishaji | - Kuandaa mazungumzo na wanasiasa ili waunge mkono zoezi la Sensa ya Majaribio.<br>- Kukaa na wanasiasa na kuzungumzia kuacha kupotosha wafuasi wao kuhusu zoezi la Sensa |
| 5.Uajiri wa Makarani na wasimamizi wa Sensa na Mafunzo yao | -Kuajiriwa kwa baadhi ya Makarani wa Kuhesabu na Wasimamizi wasiokuwa na sifa katika baadhi ya maeneo<br><br>-Kukiukwa kwa sifa za uajiri wa makarani na wasimamizi wa Sensa<br><br>-Ushirikiano hafifu na taasisi nyingine za Serikali | - Viongozi wa Siasa<br>- Kamati ya Wataalamu<br>- Watendaji wa Mikoa na Wilaya.<br>- Wakuu wa Wizara, Idara na Taasisi.<br>- Ofisi za Sensa<br>-<br>- Wizara ya Fedha na Mipango | - Uajiri wa Makarani wa Kuhesabu na Wasimamizi wenye sifa ni muhimu katika kupata takwimu za Sensa zilizo bora na zinazokubalika<br>- Sensa ni mchakato shirikishi kwa maendeleo ya wote<br><br>- Sensa ni mchakato shirikishi wa ukusanyaji wa takwimu kwa mipango ya maendeleo ya wote | **Mjumbe:**<br>- Ofisi za Sensa (NBS na OCGS)<br>- Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>- Kamati za Sensa za Mikoa na Wilaya.<br><br>**Njia:**<br>- Mkutano na vikao vya uhamasishaji. | - Kutayarisha Mwongozo wa uajiri<br>- Kuhamasisha taratibu za uajiri lazima zifuatwe.<br><br>Kuendesha vikao vya mashirikiano na wadau zikiwemo taasisi nyingine za Serikali.<br>- kupitia mpango shirikishi kuwepo na ushirikiano na ushirikishwaji wa taasisi husika ili kuimarisha shughuli za ukusanyaji wa |

| Tukio | Tatizo/ Changamoto | Mlengwa/ Mhusika | Maudhui ya Ujumbe | Njia ya mawasiliano | Hatua za Kuchukua |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | takwimu utaohakikisha utekelezaji wa mipango na sera bora za maendeleo. |
| 6. Kuhesabu watu | -Muda wa Kuhesabu watu kwa kutumia dodoso refu (siku saba) hautoshi. | -Kamati ya wataalamu ya Sensa.<br>-Ofisi za Takwimu, NBS na OCGS. | -Kuimarisha ubora wa ukusanyaji wa taarifa za kila siku utapunguza idadi ya maswali katika Dodoso la Sensa | **Mjumbe**<br>- Kamati ya wataalamu wa Sensa.<br>- Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.<br>- Ofisi za Takwimu za NBS na OCGS.<br>**Njia:**<br>- Mikutano ya Kamati ya Sensa. | -Kuhamasisha taasisi za takwimu na taasisi nyingine kwa lengo la kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa takwimu za kila siku ili kupunguza wingi wa maswali katika madodoso ya Sensa na hatimae kupata muda muafaka wa ukusanyaji wa taarifa za Sensa |
| | -Baadhi ya jamii za vijijini kushindwa kuelewa lugha ya Kiswahili | -Kamati ya wataalamu ya Sensa<br>-Kamati za Sensa za Mikoa na Wilaya<br>-Wakalimani wa lugha za alama. | Kuhamasisha matumizi ya lugha ya Taifa ili kujenga umoja na maendeleo ya kitaifa | **Mjumbe:**<br>- Kamati ya wataalamu wa Sensa.<br>- Kamati za Sensa za Mikoa na Wilaya.<br>- Viongozi wa Serikali za Mitaa<br>**Njia**<br>- Mikutano ya mashauriano ya wanajamii. | - Kuainisha maeneo ambayo yana watu wanaoshindwa kuelewa lugha ya Kiswahili.<br>- kuhamasisha uajiri wa makarani wa kuhesabu wanaotokea katika maeneo husika. |
| | -Tabia ya baadhi ya Makarani na Wasimamizi wa Sensa Kukiuka miko ya utunzaji wa usiri katika baadhi ya matukio. | -Viongozi wa Serikali ya Mitaa<br>-Kamati ya wataalamu wa Sensa<br>-Wasimamizi na Makarani wa Sensa<br>-Wananchi | - Utunzaji siri kwa taarifa za Sensa ni ngao ya mafanikio kwa programu za Sensa na mipango ya maendeleo ya Taifa ya sasa na baadaye<br>- Kutunza siri katika maeneo ya kuhesabu ni njia ya | **Mjumbe:**<br>-Viongozi wa Serikali za Mitaa<br>- Kamati ya wataalamu wa Sensa<br>- Wasimamizi na Makarani wa Sensa.<br>**Njia:**<br>Mikutano na Vikao vya uhamasishaji | - Viongozi wa Serikali za Mitaa, Wasimamizi na Makarani wa Sensa wanalazimika kufuata misingi ya utunzaji wa siri wakati wa zoezi la Sensa.<br>Kuwajengea Imani wananchi kuwa taarifa zao zitatunzwa na kubaki kuwa siri |

| Tukio | Tatizo/ Changamoto | Mlengwa/ Mhusika | Maudhui ya Ujumbe | Njia ya mawasiliano | Hatua za Kuchukua |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | kujenga uaminifu na hivyo kupata data bora za Sensa | | |
| | -Baadhi ya watu kutotoa majibu kwa kuhofia kutozwa kodi na kufilisiwa mali zao<br><br>-Changamoto ya kuwafikia watu walio katika maeneo yenye ugumu wa kufikika | - Kamati ya wataalamu wa Sensa.<br>- Viongozi wa Serikali za Mitaa.<br>- Kamati za Sensa za Mikoa na Wilaya. | -Taarifa zinazokusanywa ni kwa madhumuni ya shughuli za kitakwimu tu na zitabaki kuwa siri. | **Mjumbe:**<br>- Kamati ya wataalamu wa Sensa.<br>- Viongozi wa Serikali za Mitaa.<br>- Kamati za Sensa za Mikoa na Wilaya<br><br>**Njia**<br>- Mikutano na vikao vya uhamasishaji<br>- Vielelezo vya uhamasishaji | -kuwahamasisha na kuwajengea Imani kuwa taarifa zao zitabaki kuwa siri |
| | | Kamati Kuu ya Sensa.<br>-Ofisi za Takwimu za NBS na OCGS.<br>-Kamati za Sensa za Mikoa na Wilaya. | -Uimarishaji wa miundombinu ya maeneo yasiyofikika kirahisi ni muhimu kwa upatikanaji wa data za Sensa kwa wakati muafaka. | **Mjumbe:**<br>- Kamati Kuu ya Sensa.<br>- Ofisi za Takwimu za NBS na OCGS.<br>- Kamati za Sensa za Mikoa na Wilaya.<br><br>**Njia:**<br>- Mikutano ya mashauriano | - kuhamasisha kamati za Sensa husika kuhakikisha uimarishaji wa miundombinu katika maeneo yasiyofikika kwa urahisi |
| | -Kupoteza kumbukumbu kwa baadhi ya wakuu wa kaya wanaotakiwa kujibu dodoso. | -Kamati Kuu ya Sensa.<br>-Kamati ya wataalamu wa Sensa | -Utunzaji wa kumbukumbu za matukio katika kaya unahakikisha usahihi, uaminifu na kukubalika kwa data za Sensa.<br>-Kutenga rasilimali zaidi ili kurahisisha na kupunguza muda wa kuhesabu watu. | **Mjumbe:**<br>- Kamati ya wataalamu wa Sensa.<br>- Kamati za Sensa za Mikoa na Wilaya<br>- Viongozi wa Serikali za Mitaa | - Kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali nyingi zaidi ili kurahisisha ukusanyaji wa taarifa za Sensa<br><br>- kuhamasisha kaya kutunza na kutoa taarifa sahihi zinazohitajika kwa ajili ya zoezi la Sensa |

| Tukio | Tatizo/ Changamoto | Mlengwa/ Mhusika | Maudhui ya Ujumbe | Njia ya mawasiliano | Hatua za Kuchukua |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **Njia**<br>- Mikutano ya Sensa<br>- Nyenzo za Uhamasishaji kulingana na hali halisi ya walengwa<br>- Vyombo vya Habari | |
| | -Baadhi ya wanawake hawaruhusiwi kutoa majibu ya maswali bila ya ruhusu za waume zao. | - Viongozi wa Kijamii na Viongozi wenye Ushawishi.<br>- Viongozi wa Serikali za Mitaa<br>- Wanawake<br>- Wanaume | - wanaume wawaruhusu wanawake waweze kushiriki katika zoezi la Sensa | **Mjumbe:**<br>- Viongozi wa Kijamii na Viongozi wenye Ushawishi.<br>- Viongozi wa Serikali za Mitaa<br>**Njia**<br>- Mikutano na vikao vya uhamasishaji | - Kuongeza uelimishaji na uhamasishaji ili kuondokana na mfumo dume katika kushiriki Sensa. |
| 7.Usimamizi | - Ushirikiano hafifu kwa baadhi ya Viongozi wa Mikoa, Wilaya na Serikali za Mitaa. | -Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Serikali za Mitaa. | - Mamlaka za Wilaya na Serikali za Mitaana kamati ya uhamasishaji wana wajibu mkubwa wa kuratibu zoezi la Sensa. Sensa ni tukio la kitaifa ambalo linahitaji ushiriki wa kila mmoja, | **Mjumbe:**<br>- Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Serikali za Mitaa<br>**Njia**<br>- Mikutano na Majadiliano | - Kamati za Sensa kutengeneza na kutekeleza mashirikiano ya mtandao wa utekelezaji kazi |
| | - Makarani kutohesabu kaya zote au kupitiliza maeneo ya mipaka ya eneo la kuhesabia watu<br>- Dhana potofu ya wanasiasa ya faida za kijamii na kiuchumi | - Sekretarieti ya Sensa.<br>- -Wasimamizi na Makarani wa Sensa<br>-<br>- -Wanasiasa na Viongozi wa Serikali za Mitaa.<br>- | - Takwimu sahihi ni muhimu katika kupanga na kufanya maamuzi.<br>Wahusika wote wa masuala ya Sensa wahakikishe wanatekeleza majukumu | **Mjumbe:**<br>- Kamati ya wataalamu wa Sensa.<br>- Kamati za Sensa za Mikoa na Wilaya<br>- Viongozi wa Serikali za Mitaa. | - Kuwahamasisha wafanyakazi wa Sensa, Viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa juu ya umuhimu wa takwimu pamoja na kuwa na usimamizi wa karibu wa zoezi la Sensa .<br>- kutoa Mafunzo stahiki kwa makarani na wasimamizi kuweza kukusanya |

| Tukio | Tatizo/ Changamoto | Mlengwa/ Mhusika | Maudhui ya Ujumbe | Njia ya mawasiliano | Hatua za Kuchukua |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | sahihi pasi na kuingiza maslahi binafsi katika zoezi la Sensa | **Njia**<br>- Mikutano ya Sensa<br>- Nyenzo za Uhamasishaji<br>- Vyombo vya Habari | takwimu sahihi za Sensa katika maeneo husika |
| 8. Usambazaji wa takwimu zitokanazo na Sensa na matumizi yake | - -Usambazaji wa taarifa za Sensa kwa kiwango cha chini<br>- -kiwango kidogo cha Matumizi ya taarifa za Sensa | - Watumiaji wa taarifa wakiwemo serikali na wadau wa maendeleo<br>- Jumuiya ya Wafanyabiashara<br>- Ofisi za Takwimu, Wizara, Idara na Mashirika na Serikali za Mitaa Taasisi za Elimu ya Juu na Utafiti<br>- Asasi za Kiraia<br>- Viongozi wa dini na Taasisi za Wataalamu. | - Maamuzi mazuri yanategemea taarifa sahihi za Sensa<br>- Tumia takwimu kufanya maamuzi sahihi. | **Mjumbe:**<br>- Taasisi za Serikali, Jumuiya ya Wafanyabiashara, Asasi za Kiraia.<br>-<br>**Njia**<br>- Ripoti za Sensa.<br>- Semina za usambazaji wa taarifa za Sensa<br>- Vyombo vya Habari | - Tumia takwimu kupanga na kufanya maamuzi.<br>- Wadau watumie takwimu kupanga na kufanya maamuzi.<br>- Uandishi/uwasilishaji wa ripoti na matokeo ya Sensa uwe rafiki kwa kila kundi kutokana na uelewa wao.<br>- ripoti ziwe zinapatika kwa watu wa makundi yote kupitia njia mbali mbali za uwasilishaji.<br>- Kuhamasisha takwimu kutumia takwimu za Sensa. |

# SURA YA SABA

## MUUNDO WA KITAASISI WA MKAKATI WA UELIMISHAJI NA UHAMASISHAJI WA SENSA 2022

### 1. Utangulizi

Sura hii inaeleza muundo wa kitaasisi wa Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji ambao unalenga kuwezesha utekelezaji wa Mkakati huu. Pia, inadokeza kuhusu uratibu na usimamizi wa Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji ukiwamo uratibu wake na mifumo ya usimamizi; miundo ya kiutawala, majukumu na wajibu wa Kamati mbalimbali na hadidu zake za rejea na muundo wake.

### 2. Uratibu na Usimamizi wa Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji

Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji una azma ya kuhakikisha kuwa watekelezaji wa Mkakati wanazungumza kwa sauti moja na ujumbe unaosambazwa haubagui walengwa. Matokeo ya Mkakati huu kwa kiasi kikubwa yatasaidia kupata takwimu bora ambazo zitatumika katika kupanga, kufanya maamuzi na kutunga sera mbalimbali za maendeleo kwa manufaa ya taasisi za umma na binafsi.

Katika utekelezaji wa mkakati huu, kila ngazi ya muundo wa kitaasisi itafanya shughuli zake za uelimishaji na uhamasishaji wa shughuli za Sensa kwa lengo la kukuza mafanikio na kuepuka kupoteza rasilimali. Hii inahusisha usimamizi mzuri pamoja na uratibu wa mwenendo wa mawasiliano ndani na nje ya taasisi za Sensa.

### 3. Uratibu na Taratibu za Usimamizi wa utekelezaji wa Mkakati

Uratibu wa mkakati huu utaongozwa kuanzia ngazi ya Makamisaa wa pande zote mbili za Muungano hadi Kamati ya Uhamasishaji Sensa ngazi ya Kitongoji, Mtaa /Shehia kama inavyooneshwa kwenye mchoro hapo chini. Mwenendo wa mawasiliano utahusisha uratibu, mashirikiano, na nguvu za pamoja za utendaji kazi miongoni mwa ngazi zilizotajwa.


Taratibu za usimamizi wa mkakati huu zinajumuisha mchakato na hatua za kutekeleza ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Hatua hii inahusisha ziara za ufuatiliaji, kutembelea maeneo, usimamizi, ripoti za robo mwaka na kila mwaka, mikutano ya mapitio ya maendeleo ya robo mwaka na ya mwaka. Inahusishwa pia na mchakato wa utoaji wa maoni ambapo tatizo hutambuliwa na kupatiwa ufumbuzi. Ili kutoa mwelekeo wa uelimishaji na uhamasishaji katika ngazi zote, mkakati huu umeandaa miongozo na nyenzo zitakazotumiwa katika utekelezaji.

## Muundo na Mpangilio wa Uelimishaji na Uhamasishaji

Muundo na Mpangilio wa utekelezaji wa Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji utakuwa kama ifuatavyo:-

i. Makamisaa wa Sensa;
ii. Sekretarieti ya Taifa ya Sensa;
iii. Kitengo cha Uelimishaji na Uhamasishaji;
iv. Kamati ya Taifa ya Uhamasishaji wa Sensa;
v. Kamati za Mikoa, Wilaya na Kata/Shehia za Uhamasishaji wa Sensa;
vi. Kikosi kazi cha Uhamasishaji wa Sensa; na
vii. Chama cha Wabunge wa Tanzania wanaohusika na masuala ya Watu na Maendeleo.

### Muundo wa Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji



## 4. Majukumu na Wajibu wa Kamati

Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji wa Sensa umetoa majukumu na wajibu kwa Kamati mbalimbali. Ni muhimu kuhakikisha utekelezaji wenye tija wa shughuli za Mkakati ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Sehemu inayofuata inaelezea majukumu na wajibu wa wajumbe wa kamati mbalimbali za Uhamasishaji.

## 5. Kitengo cha Uelimishaji na Uhamasishaji

Kitengo cha Uelimishaji na Uhamasishaji kimekabidhiwa jukumu la jumla la uelimishaji na uhamasishaji wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022. Kitengo kitakuwa na wajibu wa kuhakikisha utekelezaji mzuri wa Mkakati pamoja na kuweka mazingira wezeshi kwa wahusika wakuu kushiriki kwa ufanisi katika Uelimishaji na Uhamasishaji wa Sensa. Kitengo pia kitaratibu misaada ya kiufundi na kifedha itakayotolewa kwa ajili ya shughuli za Uelimishaji na Uhamasishaji. Kitengo cha Uelimishaji na Uhamasishaji kitakuwa ni sehemu ya Sekretarieti ya Kamati ya Taifa ya Uhamasishaji wa Sensa.

## 6. Kamati ya Kitaifa ya Uhamasishaji wa Sensa

Jukumu kuu la kamati hii ni kutoa ushauri wa kiufundi kwa Kamati Kuu ya Sensa juu ya masuala ya Uelimishaji na Uhamasishaji katika ngazi ya Taifa. Kwa hiyo, Kamati ya Kitaifa ya Uhamasishaji ya Sensa itakuwa ni kamati ya kitaalamu ya Sekretarieti ya Sensa. Kamati hii itakuwa na majukumu yafuatayo:

i) Kuwezesha utekelezaji wa Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji kupitia wito wa uungwaji mkono kutoka kwa wadau (Serikali, Wadau wa Maendeleo, Jumuiya ya Wafanyabiashara na Asasi za Kiraia);

ii) Kutoa mwongozo wa kitaalamu juu ya Uelimishaji na Uhamashishaji wa Sensa.

iii) Kuishauri Sekretarieti ya Sensa juu ya utekelezaji wa Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji.

iv) Kufuatilia utekelezaji wa Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji kwa kutembelea maeneo ya Sensa, kufanya mikutano ya robo mwaka na kila mwaka na mikutano ya mapitio ya kazi.

v) Kuwasiliana na Sekretarieti ya Sensa kutoa taarifa kwa Mawaziri wanaohusika na Sensa.

**Wajumbe wa Kamati ya Taifa ya Uhamasishaji wa Sensa**

Wajumbe wa Kamati ya Taifa ya Uhamasishaji wa Sensa ni kama ifuatavyo:-

i. Makamisaa wa Sensa;
ii. Mkuu wa Sekretarieti ya Sensa;
iii. Mkuu wa Kitengo cha Uelimishaji na Uhamasishaji;
iv. Wawakilishi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar;
v. Wawakilishi kutoka Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
vi. Wawakilishi kutoka Wizara ya Fedha na Mipango (Bara na Zanzibar);
vii. Mwakilishi kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo;
viii. Mwakilishi kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni, Vijana na Michezo-Zanzibar;
ix. Wawakilishi kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali;
x. Wawakilishi kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia;
xi. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA);
xii. Tume ya Utangazaji Zanzibar;
xiii. Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Vyombo vya Habari;
xiv. Wawakilishi kutoka Jukwaa la Wahariri Tanzania (Bara na Zanzibar);
xv. Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge wa masuala ya Watu na Maendeleo;
xvi. Mwakilishi wa Kikosi kazi cha Uelimishaji na Uhamasishaji wa Sensa;
xvii. Mwakilishi wa Jumuiya ya Wafanyabiashara;
xviii. Mwakilishi wa Wadau wa Maendeleo;
xix. Mwakilishi wa Asasi za Kiraia;
xx. Wawakilishi wa Viongozi wa dini;
xxi. Mwenyekiti wa Kituo cha Demokrasia Tanzania.

## 7. Kamati za Uhamasishaji za Mikoa na Wilaya

Muundo wa Kamati za Uhamasishaji za Mikoa na Wilaya unaakisi muundo wa Kamati ya Taifa ya Uhamasishaji wa Sensa isipokuwa unatofautiana katika aina ya wajumbe na hadidu rejea zao. Kamati hizi zitakuwa na jukumu la utekelezaji wa shughuli za uelimishaji na uhamasishaji katika ngazi husika za kiutendaji. Kamati za Sensa za Mkoa na Wilaya pia zitakuwa Kamati ya uelimishaji na uhamasishaji wa Sensa ya Mkoa na Wilaya na itakuwa na majukumu yafuatayo:-

i. Kuwaratibu wadau wote muhimu kwenye Mkoa na Wilaya katika kutekeleza shughuli za uelimishaji na uhamasishaji walizopewa za matayarisho ya Sensa, Wakati wa Sensa na Baada ya zoezi la Sensa.

ii. Kuhakikisha kuwa nyenzo zote za uelimishaji na uhamasishaji zinapatikana kwa wakati kutoka Sekretarieti ya Sensa;

iii. Kuishauri Kamati ya Taifa ya Uelimishaji na Uhamasishaji wa Sensa juu ya masuala yanayohusiana na uelimishaji na uhamasishaji na kutoa mrejesho juu ya utekelezaji wa shughuli;

iv. Kutayarisha taarifa za kila mwezi, robo mwaka na ripoti nyingine za utekelezaji;

v. Kutoa taarifa juu ya utekelezaji wa Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji;

vi. Kukusanya taarifa za mara kwa mara za utekelezaji wa shughuli za Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji katika ngazi ya Mkoa na Wilaya; na

vii. Kufanya shughuli nyingine za Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji kama itakavyoagizwa na Mkuu wa Sekretarieti ya Sensa

**Wajumbe wa Kamati ya Uhamasishaji ya Mkoa na Wilaya**

i. Wabunge wa Bunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi;

ii. Mratibu wa Sensa wa Mkoa na Wilaya;

iii. Mwakilishi wa Katibu Tawala wa Mkoa na Wilaya;

iv. Mwakilishi kutoka Idara Elimu ya Mkoa na Wilaya;

v. Mwakilishi kutoka Idara ya Utamaduni;

vi. Wawakilishi kutoka Chama cha Wamiliki wa Vyombo vya Habari katika ngazi ya Mkoa na Wilaya na Umoja wa Redio Jamii kutoka katika kila Mkoa;

vii. Mwakilishi kutoka vyombo vya Habari/klabu za waandishi wa habari kutoka katika kila Mkoa;

viii. Wawakilishi kutoka makundi ya kidini;

ix. Maafisa wa Habari wa Mkoa na Wilaya; na

x. Wawakilishi kutoka vikundi vya Utamaduni na Sanaa.

## 8. Kamati za Uhamasishaji wa Sensa za Serikali ya Mtaa na Shehia

Kamati hii itakuwa na kazi zifuatazo:-

i. Kushirikiana na kamati za Mikoa na Wilaya ili kufanikisha zoezi la Uelimishaji na Uhamasishaji katika ngazi ya Mitaa na Shehia;

ii. Kuhamasisha jamii kuunga mkono na kushiriki katika Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022;

iii. Kufuatilia na kuweka kumbukumbu za maendeleo ya shughuli za Sensa katika ngazi ya Mtaa na Shehia; na

iv. Kutoa ripoti za kila mwezi juu ya Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji katika Kata/Shehia na kuiwasilisha katika Wilaya zao.

**Muundo**

i. Mtendaji wa Kata/Sheha;

ii. Diwani;

iii. Wenyeviti wa Vijiji na vitongoji;

iv. Watendaji Wakuu wa Vijiji;

v. Maafisa Maendeleo ya Jamii;

vi. Mratibu wa Elimu wa Kata;

vii. Mwakilishi wa Taasisi za Kidini; na

viii. Mwakilishi kutoka Taasisi za Kiraia.

## 9. Chama cha Wabunge wa Tanzania Juu ya Masuala ya Watu na Maendeleo

Chama cha Wabunge wa Tanzania Juu ya Masuala ya Watu na Maendeleo ni kiungo baina ya mashirika yanayojihusisha na watu au taasisi zinazohusiana na masuala ya idadi ya watu na wabunge.

Chama cha Wabunge wa Tanzania Juu ya Masuala ya Watu na Maendeleo ni chombo muhimu kwa msaada wa kisera kwa masuala ya Sensa katika Bunge na Baraza la Wawakilishi ili kupata uungwaji mkono wa Serikali na ahadi kwa zoezi la Sensa.

Kwa hiyo ni muhimu kwa wanachama wa chama hicho kupewa taarifa juu ya masuala ya Sensa pamoja na maarifa juu ya uelimishaji na uhamasishaji wa shughuli mbalimbali za Sensa ikiwemo uhamasishaji wa upatikanaji wa rasilimali fedha.

Chama cha Wabunge wa Tanzania kuhusu Masuala ya Watu na Maendeleo kitakuwa na majukumu yafuatayo:

i. Kujenga uhusiano kati ya Bunge na Sekretarieti ya Sensa;

ii. Kufanya shughuli za uhamasishaji kwa wabunge na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi;

iii. Kushirikiana na Kamati ya Kitaifa ya Uelimishaji na Uhamasishaji wa Sensa katika juhudi za kutafuta rasilimali za Sensa kutoka kwa Serikali, Wadau wa Maendeleo na wadau wengine muhimu kama vile Jumuiya ya Wafanyabiashara na Mashirika ya Kiraia; na

iv. Kufanya kazi kwa karibu na Sekretariati ya Taifa ya Sensa juu ya masuala ya Sensa yanayohitaji maamuzi ya Bunge.

## 10. Kikosi Kazi cha Uelimishaji na Uhamasishaji

Kikosi Kazi kitakuwa na majukumu yafuatayo:-

i. Kushawishi vyombo vya habari kuunga mkono uelimishaji na uhamasishaji wa Sensa katika ngazi ya Taifa, Mkoa, Wilaya hadi ngazi ya Kitongoji/Mtaa/Shehia

ii. Kuhakikisha kuna utolewaji wa habari za kina juu ya shughuli za Sensa;

iii. Kushiriki katika Kamati za Uelimishaji katika ngazi zote;

iv. Kufuatilia taarifa za vyombo vya habari kuhusu shughuli za Sensa;

v. Kuratibu shughuli za uhamasishaji na uelimishaji wa Sensa zinazofanywa na Makamisaa wa Sensa;

